# Nipashe

Alhamisi Machi 21, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579871

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Aliyebambikwa kesi ya mauaji afunguka mazito

UKURASA 3




UKURASA 13

# Korti yasimamisha uchaguzi Arumeru

• **Ni** ule wa kujaza nafasi ya Nassari, yampa AG siku saba kutoa utetezi uamuzi wa Spika Ndugai... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 7**

### AZANIA YANUNUA RASMI BANK M

BENKI ya Azania imetangaza rasmi kuchukua mali na madeni ya iliyokuwa Bank M ambayo...

**UKURASA WA 26**

### WABUNGE WA CHADEMA KUTETEA MAHABUSI, WAFUNGWA MJENGONI

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimewaelekeza wabunge wake wasimame kidete kwenye cha...


## Marekani yamwagia wanawake bil. 1.1/-

UKURASA 2



NASSARI NDUGAI



UK.2

## Mashine feki EFD zazagaa kila kona

MICHEZO NIYONZIMA: NAIONA SIMBA FAINALI CAF UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

# Marekani yawamwagia wanawake bil. 1.1/-

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa (Usaid), imetoa msaada wa Dola za Marekani 500,000 sawa na Sh. bilioni 1.1 kusaidia wanawake 500 watakaotaka kugombea uongozi.

Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, alisema hayo jana, wakati wa uzinduzi wa mradi wa awamu ya pili uliolenga kuwajengea uwezo wanawake kupata uongozi katika nyanja mbalimbali ikiwamo katika siasa.

Dk. Patterson alisema mchango huo unajumuisha mafunzo ya masuala ya kisiasa na michakato ya uchaguzi, kutimiza malengo ya muda na jinsi ya kumudu ratiba za chama na uteuzi.

Alisema serikali ya Marekani itachangia kulea na kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa

INAENDELEA UK. 8



Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Zanzibar, Salum Mwalimu, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakiitaka serikali kushughulikia tatizo la msongamano wa mahabusi gerezani, kufuatia rai iliyotolewa na mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Korti yasimamisha uchaguzi Arumeru

**Na Waandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dodoma imesimamisha mchakato wa uchaguzi mdogo katika Jimbo la Arumeru Mashariki hadi shauri la kutoridhishwa na uamuzi wa Spika wa Bunge, Job Ndugai, litakaposikilizwa.

Shauri hilo limefunguliwa katika mahakama hiyo na aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Joshua Nassari (Chadema).

Vilevile, mahakama hiyo imetoa siku saba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kuwasilisha majibu ya madai ya Nassari ambaye anapinga uamuzi wa Spika Ndugai kumvua ubunge.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Naibu Msajili, Dynes Lyimo, alithibitisha Nassari kufungua shauri hilo katika mahakama hiyo.

Alisema uamuzi wa kusimamisha mchakato wa uchaguzi na kumtaka AG kujibu madai ya Nassari, ulitolewa jana na Jaji Latifa Mansour aliposikiliza shauri hilo namba 22/2019 lililofunguliwa Machi 18, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Lyimo, Jaji Mansour alisema Nassari aliomba kibali cha kufungua kesi ya msingi ili kutengua uamuzi wa Spika Ndugai kumvua ubunge wake.

Lyimo alisema kesi hiyo imepangwa kusikilizwa Machi 27, mwaka huu. Katika kesi hiyo, Nassari anatetewa na mawakili watatu ambao ni Hekima Mwasipe, Jonathan Mndeme na Fred Kalongo, huku Upande wa Jamhuri ukiwakilishwa na Wakili Masonga Kawahanda.

Machi 14, mwaka huu, Spika Ndugai alimwandikia barua Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), akieleza kuwa Nassari amepoteza sifa za kuendelea kuwa mbunge kutokana na kutohudhuria mikutano mitatu ya Bunge bila ruhusa na taarifa kwa Spika.

Taarifa ya Bunge kuhusu Spika kumvua ubunge Nassari ilieleza kuwa mwanachama huyo wa Chadema hakuhudhuria mikutano mitatu mfululizo iliyofanyika Septemba 4-14, mwaka jana, Novemba 6-16, mwaka jana na Januari 29 hadi Februari 9, mwaka huu.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uamuzi huo umefikiwa kwa kuzingatia Ibara ya 71(c) ya Katiba, inayosema iwapo mbunge hatahudhuria vikao vitatu mfululizo, ataondolewa katika nafasi hiyo.

Juzi, NEC iliiambia Nipashe kuwa inasubiri muda ufike ndipo itangaze rasmi kuwa Jimbo la Arumeru Mashariki liko wazi na kuanza mchakato wa uchaguzi mdogo.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Athuman Kihamia, alisema wamepokea barua ya Spika Ndugai akiwaarifu kuwa jimbo hilo liko wazi.

"Tumeshapokea barua ya Spika na hivi karibuni tutatoa taarifa kwa umma juu ya hatua inayofuata kuhusiana na jimbo hilo," Kihamia alisema.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, jimbo au kata inapotangazwa rasmi kuwa iko wazi, uchaguzi unatakiwa kufanyika ndani ya siku 90.

***Imeandaliwa na Paul Mabeja (DODOMA) na Enock Charles (DAR)**

# Mashine feki EFD zazagaa kila kona

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema imebaini kuzagaa kwa mashine feki za EFD ambazo zinatumiwa kutoa risiti feki maeneo mbalimbali nchini hali ambayo inaikosesha serikali mapato.

Aidha, imesema wapo wafanyabiashara wanaotoa risiti za viwango vidogo tofauti vya kiasi halisi ili kukwepa kodi, jambo ambalo ni uhujumu uchumi.

Hayo yalisemwa jana na Kamishna Mkuu wa TRA, Charles Kichere, wakati akifungua mkutano wa washauri wa kodi Dar es Salaam pamoja na mtoa mada ambaye pia Ofisa Msaidizi wa Kodi wa Mamlaka hiyo, Honest Njau.

Mkutano huo uliofunguliwa na Kichere, ulijadili changamoto na uboreshaji katika masuala ya ukusanyaji wa kodi ili kuinua ulipaji wa kodi kwa hiari.

Akiwasilisha mada kuhusu mashine za EFD, Njau alisema ziko mashine feki (ghost machines) ambazo hutumika kutoa risiti feki na kuikosesha serikali mapato.

Njau alisema wanazitambua mashine hizo kutokana na aina ya risiti zinazotolewa kuwa na maandishi yenye ukubwa tofauti na zile sahihi na kwamba hatua zinachukuliwa kila wanapobainika.

Akifungua mkutano huo, Kichere alisema wafanyabiashara wengi wanapofanya mrejesho wa kodi, ndipo katika ukaguzi TRA inabaini

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
19 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 27-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Mbeya kuelekea Dar -Es-Salaam**, gari hizo zenye namba za usajili:
   **T 133 CCP / T 574 BZB / T 296 CZS / T 900 BAZ**
   **T 636 DFA / T 837 DJB / T 221 BYM / T 887 DJB**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 27 |
| **Upana** | - | mita | 2.84 |
| **Kimo** | - | mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika: **Mbeya hadi Dar-Es-Salaam** Kupitia Iringa, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

215129402

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
19 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 27-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Mutukula kuelekea Tunduma**, gari hilo lenye namba za usajili:
   **T 624 DFA / UAS 392 F**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 23 |
| **Upana** | - | mita | 2.84 |
| **Kimo** | - | mita | 5.20 |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Buzwagi** Kupitia Dodoma, Gari Litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

215129402

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## HABARI KITAIFA

# Aliyebambikwa kesi mauaji afunguka mazito

**Na Romana Mallya**

MFANYABIASHARA Mussa Sadiki aliyebambikwa kesi ya mauaji na Jeshi la Polisi mkoani Tabora, ameeleza alivyokamatwa na askari wa jeshi hilo, kunyang'anywa mali zake hadi kuingizwa mahabusu gerezani.

Wiki iliyopita, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), ilifichua jinsi baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi walivyombambika kesi ya mauaji mkazi huyo wa Tabora baada ya kumpoka mali zake.

Akisimulia tukio hilo, mfanyabiashara huyo alidai kuwa Juni 11, mwaka jana, alifika Tabora majira ya saa saba mchana akitokea Dar es Salaam. Sadiki alidai kuwa baada ya kufika mjini Tabora, alipanda gari kwenda Soko la Kachome mkoani humo kwa lengo la kukutana na mtu aliyekuwa akimdai Sh. milioni 1.6.

"Nilikutana na mdeni wangu, lakini aliniambia nimsubiri kidogo anakwenda kutoa fedha kwa wakala, muda mfupi nikamwona askari polisi ambaye alinifuata na kuniuliza kama mimi ndiye Mussa Adamu Sadiki na baada ya kumjibu, nilikamatwa na kufungwa pingu," Sadiki alidai.

Mfanyabiashara huyo aliongeza: "Nilinyang'anywa mali zangu na kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi Tabora, nilipowauliza kesi gani inayonikabili, niliambiwa niendelee kukaa huko kituoni na nitajua wakati wakiendelea kuifuatilia.

"Nikiwa kituoni hapo, alifika askari ... (alitaja jina la askari polisi) majira ya saa 8:00 mchana ili kuhakiki mahabusi. Nilimuuliza huyo afande, 'nina kesi gani iliyoniweka humo ambayo hadi siku hiyo ilikuwa ni wiki ya pili?' Aliniambia ninashtakiwa kwa kosa la kuvunja na kuiba ofisini."

Sadiki alidai kuwa siku tano baada ya kupewa taarifa za kwamba anakabiliwa na tuhuma za kuvunja na kuiba, alichukuliwa na kupandishwa ghorofani huku akiwa amefungwa pingu mikono na miguu.

Alidai kuwa akiwa huko, alilazimishwa ashike kibao kilichoandikwa 'unyang'anyi wa kutumia nguvu' na akapigwa picha akiwa amekishika.

Alidai kabla ya kupigwa picha hiyo, alihoji kwanini wanamfanyia hivyo, huku wakiwa wamemfunga pingu, wakati watuhumiwa wengine hawakufanywa hivyo.

"Niliambiwa nikishike kibao, nilitii wakanipiga picha na baadaye tulirudishwa kituoni, nilichukuliwa maelezo na baada ya muda nikafikishwa mahakamani, lakini nikaambiwa mashtaka yanayonikabili sitakiwi kujibu chochote," Sadiki alidai.

"Nilisomewa mashtaka ambayo nilishtakiwa kwa kumuua Thomas Jacob mnamo Juni 5, barabara ya kwenda Kazima, Ipuli mjini Tabora, niliambiwa nisijibu lolote. Juni 29, nikapelekwa gerezani."

Sadiki alidai kuwa, awali akiwa kituo cha polisi, alikutana na mshtakiwa mwingine, Edward Nduli, ambaye baadaye aliachwa huru.

"Nilimkuta akiwa na kesi ya kuvunja na kuiba Kituo cha Polisi mjini (Kituo Kikuu cha Polisi Tabora). Nikiwa gerezani wiki mbili mbele, mahabusi mmoja alinitafuta na akanitolea jalada la kesi ambalo linaonyesha mimi ni mshtakiwa namba moja na mshtakiwa namba mbili ni Edward Nduli," Sadiki alidai.

Alidai wakati kesi hiyo inaendelea mahakamani, alikuwa akifuatilia mali zake alizopokwa na askari polisi ambazo ni Sh. 788,000, simu tatu na nguo alizonunua Kariakoo jijini Dar es Salaam na kwamba alikuwa na nyaraka za kuthibitisha ununuzi wa vitu hivyo.

"Hizi mali nilinyang'anywa na askari ambao ni .... (alitaja majina ya askari polisi watatu)," mfanyabiashara huyo alidai.

Sadiki alidai anakumbuka akiwa mahakamani, hakimu alimwambia hawezi kuandika madai ya vitu vyake kwenye faili la kesi ya mauaji na kumtaka atumie mbinu nyingine.

"Hakimu alinieleza niandike barua kwenda kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa na Mpelelezi wa Wilaya. Pamoja na kufanya hivyo, sikupata majibu hadi nimeachiwa kwa agizo la Rais John Magufuli, namshukuru sana kwa utendaji wake wa kazi.

"Wamefuatilia suala langu, wamenibambika kesi ambayo sijaifanya, sasa hivi najisikia nina amani, nipo huru nimeachiwa na sina kesi ya mauaji niliyopewa kwa lengo la kuninyang'anya fedha zangu, namshukuru Rais Magufuli.

"Waliniambia ninashtakiwa kwa kosa la kuvunja ofisi na kuiba, lakini hata jina la ofisi hiyo sikutajiwa. Baadaye nikapigwa picha, nikaambiwa nina kosa la unyang'anyi.

INAENDELEA UK. 8



# Kanuni mpya ya uvuvi kuanza Julai Mosi

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema atahakikisha wavuvi nchini wanapata elimu ya uvuvi na kufuata sheria na kanuni zilizowekwa.

Aliyasema hayo juzi, alipokutana na wavuvi katika ukanda wa Bahari ya Hindi mkoani Tanga na kusikiliza changamoto zinazowakabili.

"Julai Mosi tunataka kanuni mpya ya uvuvi ianze kutumika ambayo itakuwa imeondoa changamoto zinazotukabili," Mpina alisema.

Alisema serikali inafanya jitihada ili kuzuia uvuvi haramu na kulinda rasilimali za wavuvi nchini na kwamba inatumia Sh. bilioni 56 kila mwaka kuagiza samaki kutoka nje ya nchi.

Waziri Mpina pia aliongoza tukio la kuteketeza vipande vya nyavu haramu 773 ambazo zilikutwa katika maeneo ya Kigombe, Moa na Tanga.

Aliwataka wavuvi kukabidhi nyavu zote chini ya milimita 10 wizarani na nyavu za kuanzia milimita nane alisema hazitaruhusiwa kutumika.

"Nyavu hizi ambazo hazitakiwi zinaua mazalia ya samaki na kuvua samaki wachanga wasioruhusiwa.

Natoa elimu kwa wavuvi kuwa, wanavua samaki ambao hawastahili matokeo yake uzalishaji unakuwa mdogo," alisema.

Alisema anayevua kutumia uvuvi haramu hatapona na mapambano yanaendelea ili kila mtu afuate sheria na taratibu zilizowekwa.

Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Daudi Mayeji, alisema sheria na taratibu zikizingatiwa kutakuwa na uvuvi wenye tija.



Meneja wa Hospitali ya Macho ya Kimataifa (The International Eye Hospital), Adam Mwatima, akiwaonyesha maeneo mbalimbali ya hospitali hiyo, mabalozi wa nchi sita zinazounda Jumuiya ya Mabalozi wa Nchi za Kiarabu walipotembelea hospitalini hapo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA NA MPIGAPICHA WETU**

# H'shauri zakaidi kutekeleza mapendekezo ripoti za CAG

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zimekuwa zikibainisha kuwa bado kuna tatizo kubwa la halmashauri kutotekeleza mapendekezo ya ukaguzi hasa kwa miaka ya nyuma.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Tixon Nzunda, alipokuwa akifungua kikao kazi cha kupokea na kuhakiki taarifa za majibu na mipango kazi ya utekelezaji wa hoja na mapendekezo ya CAG kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Alisema taarifa ya CAG kwa mwaka 2016/17, ilibainisha kati ya mapendekezo 12,703 yaliyotolewa kwa mwaka 2015/16 na mapendekezo 4,262 sawa na asilimia 34 pekee ndiyo yaliyotekelezwa kwa ukamilifu.

Hata hivyo, alisema kati ya maagizo 748 yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), maagizo yaliyotekelezwa na kukamilika yalikuwa 233 sawa na 31 pekee.

Aidha, aliwataka watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha uwezo wa ofisi za wakaguzi wa ndani ili waweze kusaidia jukumu la usimamizi thabiti wa fedha za umma.

Nzunda alisema kuwa ni wajibu wa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ndio Maofisa Masuuli, kuhakikisha wanaimarisha ofisi za wakaguzi wa ndani kwa kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya kazi, kuwapa rasilimali watu wa kutosha na rasilimali fedha.

"Mkaguzi wa ndani ni kioo cha taasisi yetu, Mkurugenzi bora hawezi kukosa kuzungumzia misingi ya utawala bora ambayo ni pamoja na kuhakikisha kuwa anajenga misingi thabiti ya usimamizi wa fedha za umma," Nzunda alisema.

Alisema kwa mujibu wa kifungu cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982, pamoja na marekebisho yake, Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa amepewa wajibu wa kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa zinakuwa na usimamizi thabiti wa fedha.

Awali, Mkurugenzi wa Kitengo cha Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Miriam Mmbaga, alisema kuwa kikao hicho kitawahusisha wakurugenzi, waweka hazina na wakaguzi wa ndani kutoka mikoa 26 na halmashauri zote 185 nchini.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuwawezesha watendaji hao kujibu hoja za CAG, kuongeza uwajibikaji katika utendaji wao wa kazi ili hoja hizo zisijitokeze tena katika halmashauri zao.

Kwa mujibu wa Mmbaga, taarifa ya CAG inaonyesha kuwa katika mwaka wa fedha 2013/14 kati ya hoja 7,921 zilizoibuliwa ni 2,330 sawa na asilimia 29 ndizo zilizopatiwa majibu.

"Kufuatia kuibuliwa kwa hoja hizo za CAG, Ofisi ya Rais Tamisemi baada ya kupokea maagizo ya Waziri Mkuu, iliwataka wakuu wa mikoa wasimamie na kujadili utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na kuchukua hatua, jumla ya watumishi 203 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa walichukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria," alisema.

Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Msaidizi anayeshughulikia Serikali za Mitaa, Mwanyika Semroki, aliwataka watendaji hao kuhakikisha kuwa wanazingatia udhibiti na usimamizi imara wa fedha za umma hasa kwa kutambua maeneo au miradi iliyo kwenye hatari ya kufanyiwa ubadhirifu.

# 'Raia wa kigeni hawaruhusiwi kumiliki ardhi'

**Na Munir Shemweta,** MKINGA

SERIKALI imesema raia wa kigeni wanaoishi nchini hawaruhusiwi kumiliki ardhi na badala yake wanaweza kufanya uwekezaji kwa kufuata sheria na taratibu za Tanzania ikiwamo kufungua kampuni.

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema hayo jana wakati wa ziara ya

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii, ilipotembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya katika kitongoji cha Jasini, Wilaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga.

Kauli ya Lukuvi inafuatia kuelezwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mahandakini, Nassoro Mbarouk, kuwa kuna baadhi ya raia wa kigeni katika eneo hilo wanamiliki ardhi na kufanya shughuli zao kama raia wa Tanzania.

Waziri Lukuvi alisema raia wa kigeni anachoruhusiwa kukifanya katika masuala ya kumiliki ardhi nchini ni kufanya uwekezaji na kusajili kampuni Brela na raia huyo hapatiwi kibali cha makazi.

Aidha, alisema katika kuhakikisha matatizo wanayopata wananchi wa Jasini yanaisha, atamwagiza Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, kuitisha kikao cha ujirani mwema na wenzao wa Kenya.

Alisema, vikao vya aina hiyo vimekuwa vikifanyika mara kwa mara katika mikoa mingine inayopakana na nchi jirani lengo likiwa kuleta maelewano baina ya wananchi wanaoishi katika maeneo ya mipakani.

Aidha, alibainisha kuwa serikali iko katika mpango wa kuhakiki mipaka na nchi jirani na zoezi limeshaanza kwa mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Serengeti na kazi hiyo itaendelea katika maeneo mengine ya mipaka ukiwamo mpaka wa Tanzania na Kenya katika eneo la Horohoro.

Awali wananchi wa Jasini waliwaeleza wajumbe wa kamati kuwa eneo lao limekuwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kukamatwa na askari wa Kenya wanapofanya shughuli zao za uvuvi, kukosekana huduma ya umeme na maji pamoja na zahanati na hulazimika kupata huduma hiyo nchi jirani ya Kenya.

Mpaka wa Tanzania na Kenya katika mkoa wa Tanga una urefu wa kilomita za mraba 104.5, kwa upande wa Wilaya ya Mkinga ni kilomita 50.5 na Wilaya ya Lushoto 53.5, huku eneo kubwa likiwa ni hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Changamoto kubwa katika eneo la mpaka huo ni kubomolewa vigingi vya mipaka, uwapo wa pori sehemu kubwa ya mpaka na uvamizi unaofanywa na wananchi wanaoishi mipakani na eneo la Jasini baadhi ya alama ziko ndani ya nyumba.

Tanzania imepakana na nchi 10 katika eneo la nchi kavu na baharini na nchi hizo ni Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Msumbiji, Comoro na Shelisheli.

**HABARI KITAIFA**

# Jafo acharukia mikoa isiyofikia lengo viwanda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameijia juu baadhi ya mikoa ambayo imeshindwa kufikia lengo la ujenzi wa viwanda 100 kila mkoa kwa mwaka na kuagiza ifikapo Juni, mwaka huu wawe wamefikia lengo hilo.

Jafo aliyasema hayo juzi jijini hapo wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa viwanda 100 kwa kila mkoa kwa kipindi kinachoishia Desemba 2018.

Waziri Jafo alionyesha kutofurahishwa na hali hiyo, huku akisema hataitaja mikoa hiyo hadi mwezi Juni kama watakuwa bado hawajafikia lengo. "Sijafurahishwa na mikoa hiyo na inajijua haijafikia malengo ya ujenzi wa viwanda 100 nawapa muda hadi mwezi wa sita mwaka huu, mhakikishe mmefikia malengo mliyowekewa, sitaitaja nimetumia busara za uongozi ingawa kiukweli sijafurahishwa sana, mkishindwa kufikia lengo nitawataja hadharani," alisema Jafo.

Waziri Jafo alisema ujenzi huo ni utekelezaji wa mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano wa mwaka 2016/2017-2020/2021, unaojikita katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, ambao kwa kuanza kila mkoa ulitakiwa kuanzisha viwanda 100.

Alisema hadi kufikia Desemba 31, 2018, viwanda vilivyokuwa vimejengwa kwa nchi nzima vilikuwa 4,777 sawa na asilimia 183.73 ya lengo la kujenga viwanda 2,600 licha ya baadhi ya mikoa kutofikia lengo.

Alisema viwanda hivyo viligawanywa katika makundi manne ambayo ni viwanda vikubwa 108, viwanda vya kati 236, viwanda vidogo ni 2,422, na viwanda vidogo kabisa 2,010, ambavyo vilikuwa vimetoa ajira kwa wananchi 36,796 kwa nchi nzima.

Aidha, Jafo aliutaja Mkoa wa Dar es Salaam kuwa ndio ulioongoza kwa upande wa mikoa iliyofanikiwa kujenga viwanda vikubwa kwa kujenga viwanda vikubwa 46 kati ya 108 vilivyojengwa nchi nzima.

"Ukifuatiwa na mkoa wa Pwani uliojenga viwanda vinane na nafasi ya tatu ikishikwa na mikoa mitatu ambayo ni Mwanza, Lindi na Simiyu ambayo kila mmoja ulijenga viwanda vikubwa saba," alisema.

Alisema mikoa na serikali za mitaa ina wajibu wa kuwatumia kikamilifu wataalamu hasa maofisa maendeleo ya jamii na maofisa biashara waliopo ili kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na upatikanaji wa malighafi za kutosha.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa wakuu wa mikoa, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alimhakikishia waziri Jafo kuwa watatekeleza maagizo hayo kikamilifu.

# Wanawake vinara matumizi bora simu

**Na Beatrice Moses**

UTAFITI umebaini kuwa wanawake wanaomiliki simu za mkononi, wanaongoza kwa matumizi mazuri ya teknolojia hiyo ikilinganishwa na wanaume.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti ya Repoa, Dk. Donald Mmari, wakati wa uzinduzi wa ripoti ya utafiti wa majukumu ya teknolojia ya simu za mkononi na maendeleo.

Dk. Mmari alisema utafiti uliofanywa umeonyesha kuwa pamoja na wanawake wanaomiliki simu kuwa wachache asilimia, lakini asilimia 70 wana matumizi mazuri.

Alisema asilimia 72 ya wanaume wanamiliki simu wakiongoza kwa matumizi ya intenreti kwa asilimia 31 wakati wanawake wanaomiliki simu ni asilimia 52.

Mmari alisema wamebaini kwamba zaidi ya mawasiliano, simu inaweza kutumika katika kusaidia jamii kupata maendeleo.

"Katika miaka ya karibuni kumekuwa na mabadiliko makubwa na ubunifu kwenye kampuni za simu, ikiwamo utoaji wa huduma za kifedha, kuanzishwa kwa programu za uelimishaji wa masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi," alisema.

Ripoti hiyo iliyoandaliwa na GSMA ikishirikisha watafiti kutoka taasisi tatu tofauti zikiwamo Repoa, Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha (FSDT) na Atamizi ya Teknohama Dar es Salaam (DTBI), inabainisha kuwa simu imeleta matokeo chanya kwa watumiaji kwa kuwa zimewasaidia kuzifikia fursa mbalimbali za maendeleo.

Akiwasilisha ripoti hiyo jana, Mmari alisema watumiaji wa simu za mkononi wameongezeka mara tano zaidi kuanzia mwaka 2007 ambapo walikuwa watumiaji milioni tano sasa wamefikia milioni 25.2.

Alisema kati ya hao pia kuanzia mwaka 2010 asilimia 18.5 zaidi ya watu milioni nane wanatumia simu za mpya zenye internet na kwamba kwa ujumla wamefikia watu karibu milioni 11 ambao hutumia interneti kwenye simu nchini mwaka hadi mwaka jana (2018).

Mkuu wa tathmini wa GSMA, Kenechi Okeleke, alisema kampuni za simu nchini zimechangia ukuaji wa uchumi kutoka Dola za Marekani bilioni 2.5 mwaka 2016 na kuwa zaidi ya Dola bilioni nne mwaka 2020 ikiwa ni zaidi ya asilimia sita ya Pato la Taifa (GDP).

Alisema kuongezeka huko kwa uchumi kutaongeza hali ya uzalishaji kwenye kampuni za simu pamoja na kuwezesha matumuzi ya simu za mkononi chini ya mtandao mpya wa 4G. Okeleke alisema kampuni hizo za simu ambazo zimewekeza Sh tilioni sita katika uendeshaji wa huduma za mtandao nchini zimechangia kwa kulipa kodi za serikali Sh. tilioni moja sawa na Dola za Marekani milioni 441. Ofisa Mtendaji Mkuu wa DTBI, Dk. George Mulamula, alisema polisi wanajitahidi kuwatahadhalisha wananchi dhidi ya wahalifu kwa njia ya mtandao ikilinganishwa na TCRA.

Alisema polisi wamekuwa wakituma ujumbe wa maandishi kwenye simu za wananchi kuwatahadhalisha kwamba wasitume fedha kwa mtu asiyemjua, wakati TCRA hawafanyi hivyo.

Dk Mulamula alisema kampuni za simu zikiendelea na ubunifu wa kuandaa programu zinazotoa mwongozo mzuri kwa jamii zitaongeza kasi ya maendeleo.

" Mfano tunaweza kuleta mfumo mwingine ambao unaweza kusaidia hata mama ntilie kujua jinsi alivyofanya biashara zake ili kubaini matumizi yake na faida anayoipata kutokana na biashara yake," alisema.


## Tanzania Pacific Logistics Ltd

**Request for Proposals (RFP)**

**Provision of Local Transport Services**

**1. Background of Tanzania Pacific Logistics Ltd :**

Tanzania Pacific Logistics Ltd (TPL) operates an Empty Container Depot facility, providing for the handling and storage of empty 20 Ft and 40 Ft containers on behalf of shipping lines.

As part of our service to the shipping lines, TPL is also responsible for the transport of empty containers from our facility, based in Kurasini, to the Dar es Salaam Port Terminals, TPA and TICTS.

We are located within close proximity of the TPA and TICTS Port Terminals.

**Round trip distances are as follows :**

- TPA 9km's
- TICTS 12km's

**2. Scope of service to be provided**

Transport of both 20 Ft and 40 Ft empty containers from our facility, based in Kurasini, to the Dar es Salaam Port Terminals, TPA and TICTS.

**3. Deliverables**

The provision of up to 20 x truck and trailer combinations, suitable for transporting both 20Ft and 40Ft empty containers, as described in the scope of service to be provided.

Ensuring that all statutory, regulatory, health and safety and insurance requirements are met and that drivers are fully capable of performing their duties within this framework.

Ensuring that all trucks and trailers are well maintained and readily available for empty container evacuations as and when required.

The provision of a sufficient number of suitably qualified, trained and experienced drivers in order to meet the 24/7 operational requirements and targets.

**4. Background and skills**

Applicants must be well experienced in the provision of container transport services and be able to provide reliable references in this regard.

**5.How to apply**

We invite suitably qualified transporters to submit proposals including references and a brief company profile as follows:

**a) Delivery in a sealed envelope**
Marked - Request For Proposals (RFP), Provision of Local Transport Services

For attention – **Mr. Adronico Emmanuel Bambanza**
Delivered at the following address :
**Kurasini**
**Plot No 35**
**Gerezani Industrial Area**
**(Next to Puma Head Office)**
**Dar es Salaam**

Or

b) Emailed to the **Mr. Adronico Emmanuel Bambanza** to the following email address :
**hrd@tpltz.com**

For further information, please contact Mr. Adronico Emmanuel Bambanza
**hrd@tpltz.com**
**0785621115**

**Proposals should be submitted by the latest, 15h00 on the 4th April, 2019.**

Applicants will be shortlisted based on their ability to deliver the required local transport services, as well as their ability to offer the required local transport services at competitive price levels.

**Local Transport Service Providers will be appointed on a non-exclusive basis.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuchukue hatua kuukabili ukame

**NI** wazi kuwa japo mamlaka za kitaalamu hazijaweka wazi, lakini katika mikoa mingi nchini kuna hofu na dalili za ukame kutokana na mvua za masika kusuasua kwa baadhi ya maeneo na hata kunyesha kwa kiasi kidogo.

Baadhi ya maeneo kama Dar es Salaam na Pwani hayakupata kabisa mvua za vuli. Hata pale, ilipotegemewa kuwa ingenyesha zaidi kwa msimu huu wa masika kuanzia Machi hadi Mei hazikuonekana, hivyo kuongeza hatari ya kuwa na kipindi kirefu cha ukame.

Mvua inahitajika kunyweshea ardhi, kujaza mito, maziwa, malambo na madimbwi. Tena ndiyo chanzo cha maji yanayotumiwa kwenye kilimo cha umwagiliaji na zaidi inahusika na kuota na kustawi nyasi ambayo ni malisho ya mifugo na wanyama pori.

Kwa hiyo, mvua inapokosekana na ukame kuchukua nafasi yake kinachoendelea ni athari kwa mnyororo huo wa kiikolojia unaotegemea mvua kuanzia watu, wanyama pori na wafugwao, ardhi na uoto wa asili.

Athari za kukosekana mvua zinafahamika kuwa ni pamoja na watu kuhitaji chakula cha msaada au chakula cha kazi. Kwa wanaotegemea maji ya mito, visima na mabwawa ni ukosefu wa maji ya kunywa. Maji ya kulisha mifugo ni tatizo linalowanyemelea wanaoishi kwenye wilaya na mikoa mikame.

Ukame pamoja na kuumiza watu una athari kwa mifugo hasa katika sehemu ambazo wanyama hawana malisho na wafugaji wanalazimika kuhama na wanyama wao. Ni dhahiri kuwa mifugo itakufa na wafugaji watalazimika kupungua wanyama wao kwa kuwauza hata kwa kiasi kidogo cha fedha au kwa hasara.

Athari za ukame zinakwenda kwenye sekta ya wanyama pori ambayo ukosefu wa nyasi na maji ya kunywa ni changamoto kubwa inayoambatana na kuwadhoofisha na hata kuwaua wanyama hawa.

Hata hivyo huu si muda wa kuangalia nyuma ni wakati wa kuanza mikakati ya kukabiliana na ukame kwa kuanza kutekeleza sera na mipango ya kuhakikisha taifa linaandaa fedha za kutosha za kununulia chakula cha ziada kiwe cha kazi au cha msaada ili watu wasiathiriwe na njaa hasa katika mikoa yenye ukame mwingi.

Si hivyo tu, inahitajika mikakati ya kuwapatia wafugaji maji kwa ajili ya wanyama wao hasa kwenye mikoa na wilaya inayotegemea malambo na mabwawa kupata maji ya kulishia na kunywesha mifugo yao.

Ni wakati wa Wakala wa Chakula wa Taifa (NFRA) kuanza utafiti ili kuzitambua sehemu ambazo zina ukame ili kuanza kuchukua hatua mapema, tunaamini kuwa akiba ya chakula iliyokusanywa mwaka 2015/2016 msimu uliokuwa na ziada ya chakula ipo na itatumiwa kusaidia maeneo yenye mahitaji.

Lakini, ni vyema pia serikali kuanza mapema kufanya sensa za kuzitambua kaya zenye uhitaji ili ziweze kuhudumiwa haraka. Kazi hiyo ilenge kuwapata na kuwasaidia wahitaji hasa wazee, wagonjwa wasiojiweza, yatima na wajane ambao hawana namna ya kupata chakula kwa kuwa hawana kipato wala uwezo wa kuzalisha.

Kwa maeneo yanayoweza kuzalisha kwa njia ya kilimo cha umwagiliaji ndiyo wakati wa kuweka mikakati na kuhimiza wananchi kuendeleza kilimo hicho.

Ikumbukwe kuwa panapokuwa na ukame ndiyo wakati kunapoibuka wanyama waharibifu kama panya, ndege jamii ya kwelea kwelea na wadudu kama viwavi wanaoharibu mazao, ni wito wetu kwa serikali na wadau kuchukua hatua stahiki kukabiliana si tu, na ukame bali pia majanga yanayoambatana na hali hiyo mbali ya hewa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Beatrice Shayo

# Kutokana na lililoanikwa, polisi ijitakatishe

**JESHI** la Polisi lina wajibu wa kuwachukulia hatua askari wake wanaoenda kinyume na maadili ya kazi yao, pia kuwapongeza watiifu, kujenga uaminifu kwa raia na kuongeza nidhamu ya jeshi.

Kumekuwapo na malalamiko ya kila mara katika vituo vyetu vya polisi, kuwa baadhi ya washtakiwa wanapofikishwa katika vituo, wanabambikwa kesi wasizozifahamu na wanapotaka kuhoji, hawapewi nafasi, baadhi wakati mwingine hata kupigwa, ili asihoji jambo lolote.

Polisi limekuwa likiwahimiza raia kufuata sheria au kutii pasipo shuruti. Hili ni jambo la msingi na sote tunalipigia makofi.

Lakini, raia tunapata kigugumizi, hasa inapotokea mikasa tena yanathibitishwa na mamlaka za kisheria za serikali, askari kuwabambikia wananchi kesi, je, kuna sheria gani inafuatwa hapo?

Je, maadili yenu ya kazi yako wapi, ambayo mnasisitizwa sana hata na viongozi wenu wa juu waliopitia awamu mbalimbali?

Najiuliza, ni sahihi mnataka raia wawakumbushe kiapo cha majukumu yenu ya kila siku, au ndiyo kwa matendo haya matuambia, baadhi mmeshayatelekeza kule chuoni?

Maswali yananielemea, Polisi unapata faida gani unapombambika kesi mshtakiwa? Au ni ulevi wa madaraka ya kazi, kwa nyie mnayoyafanya hayo?

Je, nani anayekupa jeuri ya kumbadilishia mtu makosa yake ama ni nguvu ya fedha inakufanya unasahau kiapo cha kazi yako?

Wapo ambao wana fedha hushirikiana na askari, ili kumkamata mtu kwa chuki zake na kutaka kumuweka kituo cha polisi, ili mradi kumtesa na kama hujui haki zake, anashindwa kutoa malalamiko kama ameonewa.

Suala la askari kubambika kesi kwa watuhumiwa sio jambo geni, limekuwa likilalamikiwa kila wakati na haitashangaza ama kuwashuhudia au kusikia kuwapo kwa mtu gerezani kabambikwa kesi.

Hivi karibuni tumemsikia Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Biswalo Mganga, akiianika hadharani polisi kwa kueleza askari wake walivyombambikiza kesi ya mauaji, mfanyabiashara Mussa Sadiki.

Mshtakiwa huyo aliandika barua kwa Rais Dk. John Magufuli, kupitia katika gazeti moja la kila siku, akilalamikia kubambikiwa kesi ya mauaji ambayo DPP alitaja namba yake kutokea mkoani Tabora.

Ilielezwa kuwa, mfanyabiashara huyo baada ya kukamatwa na polisi, walimnyang'anya fedha taslimu, simu ya mkononi na mali alipokuwa amenunua kwa ajili ya wakulima wakati anakwenda kufanya ununuzi.

DPP Biswalo alisema kwamba, walifuatilia malalamiko hayo na kubaini mfanyabiashara huyo alibambikwa kesi, kwa kuwa kitabu cha kuzuia wahalifu kilichopo katika kituo cha polisi, kinaonyesha mtuhumiwa alikamatwa Juni 21, mwaka jana, kwa kosa la kuvunja nyumba usiku.

Kitabu hicho kinaonyesha mlalamikaji alitolewa mahabusu Juni 29, mwaka jana na kupelekwa mahakamani na tarehe hiyo hiyo, alikofunguliwa kesi ya mauaji Namba 8/2018 ikionyesha Mei 6, 2018, akiwa barabara ya Kazima, Tabora Mjini alimuua Jackson Thomas.

Ni tukio lililoibua simanzi kwa watu, jinsi ambavyo sinema ilivyotumika katika kubadilisha mashtaka mpaka anavyokwenda mahakamani na kusomewa kesi, ambayo haipo katika maelezo ya awali.

Kupitia ukweli huo umma ambao tulipewa na DPP, dai ambalo polisi walikiri makosa, ni zaidi ya unyama uliopitiliza.

Leo hii, ni swali la kujuliza sote ni vipi kwa anayekutwa na kama haya, mhusika anaweza kujisafisha. Kimsingi na hata familia ya mhusika inapata wakati mgumu wa kujua mwelekeo na hatima ya ndugu yao, aliyekuwa gerezani. Katika tukio hilo, kumeonyeshwa uonevu uliopitiliza mtu kuwekwa katika kituo cha polisi wiki nzima kwa kesi ya kuvunja nyumba, alistahili kupatiwa dhamana matokeo yake hakupatiwa.

Niseme kwamba, ufike wakati askari polisi wafanye kazi zao kwa kufuata kiapo na sio kuwaonea wananchi huko vituoni.

Kunapokuwapo matukio ya uonevu yanayofanywa na askari, inasababisha wananchi kukosa imani na Jeshi la Polisi, picha ambayo haistahili kuonekana hata chembe.

Huko huko ndani ya polisi, tujiulize kunapokuwapo na ukakasi wa namna hii, mnamuweka katika sura na nafasi ipi Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) Simon Sirro, kuanzia kikazi na hasa kwa umma?

Ni vyema na wakati mwafaka wa ndugu zangu wa polisi, kujisafisha na mambo machafu ya vituoni, tusimbebeshe IGP na wasaidizi wake wa ngazi ya juu, lawama zisizostahili. Dawa kuu ni kubadilika, tukianza na msingi wa kiapo mwisho wa mafunzo, miongozo, kanuni na sheria zinazosimamia majukumu.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro (wa pili kushoto), akifuatilia kwa karibu utoaji wa matibabu bila malipo, wakati Dk. Alex Minja akimuhudumia mmoja wa wanafunzi waliohudhuria katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Afya ya Kinywa na Meno Duniani, yaliyofanyika kitaifa mkoani humo jana. Kushoto ni Rais wa Chama cha Wanataaluma wa Afya ya Kinywa na Meno Tanzania (TDA). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Azania yanunua Bank M

**Na Somoe Ng'itu**

BENKI ya Azania imetangaza rasmi kuchukua mali na madeni ya iliyokuwa Bank M ambayo ilitangazwa kufilisika, hivyo waliokuwa wateja wake wametakiwa kutokuwa na hofu na fedha zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Azania, Charles Itembe, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa uamuzi huo umefikiwa baada ya benki yake kukamilisha mchakato wa kukubali kufanya kazi zilizokuwa zinafanywa na Bank M kutia saini makubaliano rasmi Machi 15, mwaka huu.

Itembe alisema ununuzi wa Bank M ulifanyika baada ya maombi ya benki yake kukubaliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), huku ikiwahusisha wanahisa wake ambao ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB).

"Tunapenda kutoa tamko rasmi kuwa benki ya Azania tulitia saini rasmi mkataba wa kuinunua iliyokuwa Bank M tangu Machi 15, baada ya kukamilisha mchakato. Tumerithi mali na madeni ya iliyokuwa Bank M," alisema Itembe.

Aliongeza kuwa uamuzi huo utanusuru zilizokuwa mali na madeni ya benki hiyo na sasa waliokuwa wateja wake wataanza kupata huduma zote kupitia matawi ya benki ya Azania.

Alisema kwa uamuzi huo, benki yao sasa mtaji wake ambao ulikuwa na thamani ya Sh. bilioni 64, umeongezeka na kufikia Sh. bilioni 181 na kwamba wafanyakazi 188 wa iliyokuwa Bank M ambao mikataba yao ilikuwa hai, watachukuliwa na Azania.

"Pia tulikaribisha wanahisa wapya ili kuongeza nguvu ya kuinunua Bank M na tayari kwa uamuzi huu utafanya idadi ya matawi yetu kuongezeka kutoka 19 hadi 22. Sasa Azania ni moja ya benki kubwa," Itembe alisema.

Aliongeza kuwa benki ya Azania itaendelea na sera yake ya kufanya kazi kwa weledi, uwajibikaji na ubunifu katika kulinda mali za wateja.

Agosti mwaka jana, BoT ilitangaza kuiweka chini ya uangalizi Bank M baada ya kushindwa kuhudumia wateja wake kutokana na changamoto mbalimbali ambazo ilipitia ikiwamo tatizo la ukwasi.

# Watu wenye ulemavu kupewa viungo bandia

**Na Mwandishi Wetu**

WATU 500 wenye ulemavu kutoka mikoa mbalimbali, wanatarajiwa kuwekewa viungo bandia bure katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), jijini Dar es Salaam.

Tiba hiyo itakayotolewa MOI kwenye kambi maalum Mei, mwaka huu, itawashirikisha madaktari bingwa wa tiba za viungo kutoka hospitali za India.

Balozi wa India nchini, Sandeep Arya, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa maadhimisho ya Miaka 55 ya Ushirikiano wa Kiufundi na Kiuchumi kati ya India na Tanzania.

"Nieleze kwa ufupi kuwa ushirika baina ya India na Tanzania umefanya mambo mengi makubwa na sasa tutaweka kambi kwa ajili ya kuweka viungo bandia miguu na mikono kwa takriban wenye ulemavu 500 katika taasisi ya MOI," alisema Balozi huyo.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo wa kimaendeleo ulioanzishwa nchini mwaka 1974, unaendelea kujenga miradi mikubwa ukiwamo wa kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria hadi Tabora, Nzega, Igunga na vijiji vingine 89 vinavyopitiwa na mradi huo, kwa gharama ya Sh. bilioni 600.

"Aidha, kupitia ushirikiano huu India itatoa Sh. trilioni 1.15 kugharamia kusambaza maji katika miji 26 nchini," aliongeza.

Katika maadhimisho hayo yanayojulikana kama Indian Technical and Economic Cooperation (ITEC), Balozi huyo alisema Tanzania ni moja ya nchi zinazopokea msaada mkubwa wa kisayansi, ufundi, teknolojia na tiba kati ya mataifa yaliyo kwenye ushirikiano wa nchi za kusini.

Aliongeza kwamba serikali yake inakusudia kuendeleza elimu na tiba mtandao kwa hiyo imependekeza kutoa elimu mtandao kwa vyuo vikuu vitano vitakavyobainishwa.

"Na pia tumependekeza kutoa matibabu mtandao 'tele-medicine' katika hospitali tano. Tunatarajia kukamilisha makubaliano hayo karibuni." Alisema Balozi Arya.


Akizungumza katika maadhimisho hayo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Profesa James Mdoe, alisema idadi ya Watanzania walionufaika na mafunzo ya kitaalamu kupitia ushirikiano huo yameongezeka kutoka 24 mwaka 1972 hadi 5,000 mwaka jana.

"Tanzania ni miongoni mwa marafiki wa India wanaonufaika na msaada wa ITEC. Kwa miaka mitano iliyopita tumepata nafasi 2,369 za masomo. Ninaishukuru India kwa msaada huo," alisema Prof. Mdoe.

Aliwataja wanufaika hao kuwa ni pamoja na wizara, Tume ya Sayansi na Teknolojia, Wakala wa Umeme Vijijini (REA), hospitali, vyuo vikuu na halmashauri za wilaya na za miji.

"Mwaka jana kupitia ushirikiano huu India ilitoa vifaa vya kisasa vya kutibu saratani katika Hospitali ya Rufani ya Bugando, msaada huo umesaidia kugundua na kutibu kansa kwa kuwa Kanda ya Ziwa ina wagonjwa wengi wa saratani," alisema Mdoe.

CAPITAL RADIO
POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

# Mashine feki EFD zazagaa kila kona

INATOKA UK. 2

risiti feki za EFD, jambo ambalo linaonyesha kuna vishoka wa kutengeneza risiti hizo.

"Mfanyabiashara anaeleta madai ya kodi ya mabilioni ya fedha lakini ukifuatilia kwa kina unakuta fedha anayodai ni ndogo na zilizobakia ni risiti feki," alibainisha na kuongeza:

"Mtu analeta madai ambayo hayapo, anataka kuchukua kiasi cha fedha tulichokusanya, hii ni sawa na wizi, anaiibia serikali. Lakini ukifuatilia washauri wa kodi wamezipitisha kuwa ni madai halali, ndiyo maana tunasema kwa sasa tutawaripoti kwenye vyombo vyao vya kitaaluma," alibainisha.

Aidha, alisema TRA imebaini kuwa mashine za EFD hazifanyi kazi inavyotakiwa kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanadanganya kwa kutoa risiti zisizo sahihi.

"Tumebaini wako baadhi ya wafanyabiashara wanafanya mauzo ya Sh. 800,000, lakini wanatoa risiti ya Sh. 500,000 au chini ya hapo, lengo ni kukwepa kodi. Hii si sahihi kabisa na wanahujumu uchumi," alisema Kichere.

Alisema jambo hilo halikubaliki kwa kuwa mashine hizo zimetolewa kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara lakini wanazitumia kuhujumu, ili TRA isipate kodi yoyote na kwamba uchunguzi unaendelea ikiwamo kuwakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola wanaofanya mtindo huo.

Aidha, alisema wako washauri wa kodi ambao wanaleta marejesho ambayo hayako sahihi na kwamba TRA imeshawabaini na hatua za kisheria zitachukuliwa baada ya kufikishwa kwenye kamati.

Kamishna huyo alisema baadhi ya wahasibu wa wafanyabiashara nchini wanahujumu uchumi kwa kutengeneza vitabu na hesabu feki ili kukwepa kulipa kodi.

Kichere alisema wahasibu hao huwa na vitabu vya kupeleka benki, TRA na halmashauri vyote vikiwa na mahesabu tofauti.

"Katika ukaguzi wetu tulimkuta mhasibu mmoja ana vitabu vitano ambavyo vyote kwa mwaka mmoja vina hesabu tofauti. Cha mauzo ya Sh. bilioni 142, kingine Sh. bilioni 80 na kinachokuja TRA Sh. bilioni 18," alisema na kuongeza:

"Kuna wahasibu sita tumewaripoti kwenye Bodi ya Wahasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA) kama chombo chao cha kitaaluma ili wachukue hatua," alisema.




Kijana muosha vioo vya magari akidandia lori la mafuta lililoko kwenye mwendo katika Barabara ya Mandela, eneo la Ubungo Darajani, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri aipa neno Ewura upimaji maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) kuwa na mfumo utakaotumika kupima gharama za maji kuendana na nishati inayotumika katika uzalishaji.

Amesema hayo jijini Dodoma katika Wiki ya Maji na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga imepata tunzo kwa kuwa mamlaka bora katika huduma ya majisafi, wakati Mwanza imepata tunzo katika huduma ya uondoaji majitaka.

Prof. Mbarawa alisisitiza bei za maji zifanyiwe tathmini, kwa kigezo cha nishati inayotumika kwa uzalishaji iwapo ni jua, umeme au huduma ya maji kutolewa kwa urahisi.

Alisema imebainika gharama za maji maeneo ya vijijini ni kubwa kuliko mijini.

Aliitaka Ewura pamoja na kudhibiti inatakiwa iangalie namna bora ya kuikuza sekta ya maji, kwa sababu huduma ya maji ikikua, mamlaka hiyo itafanya kazi zaidi kuwezesha wananchi kupata huduma bora.

Aidha, Prof. Mbarawa alisema mamlaka hiyo inatakiwa kuwa na programu ya kuwajengea uwezo wahandisi na wataalamu wa maji katika eneo la utawala na menejimenti ili watoe huduma vizuri zaidi kwa wananchi.

Aliitaka mamlaka hiyo kufanya utafiti kujua umeme na dawa za kutibu maji kwa lita moja vinatumika kwa kiasi gani ili kuangalia namna bora ya kuagiza dawa za kutibu maji kwa pamoja ili kupunguza gharama.

Prof. Mbarawa alisema ni muhimu kuwa na mfumo wa kuonyesha hali halisi ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi kwa muda wowote.

Awali, akiongea kuhusu huduma za maji, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema pamoja na mamlaka za maji kufanya biashara, uhalisia wa kinachofanyika ni huduma kwa wananchi hivyo taasisi nyingine zielewe na kuzingatia hilo.

# Aliyebambikwa kesi ya mauaji afunguka mazito

INATOKA UK.3

"Niliandika barua kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri Mkuu, Waziri wa Katiba na Sheria na kwa Rais Magufuli ambayo haikumfikia, lakini lilifika gazeti na Mwendesha Mashtaka (DPP) alikuja gerezani na kuniomyesha gazeti," Sadiki alidai.

Mfanyabiashara huyo alidai aliandika barua alipozipeleka ofisi ya Magereza, lakini aliambiwa hawana mamlaka ya kuzichukua na kuzipeleka kwa waziri.

"Walinishauri nifuatilie kwa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa (RCO) au Kamanda wa Polisi Mkoa. Nilizuiliwa na RCO nisiongee na waandishi wa habari mpaka atakaponikabidhi fedha nilizokuwa nadai. Nimekabidhiwa fedha, lakini vitu vingine nilivyokuwa navidai sijapewa," Sadiki alidai.

Alitaja vitu anavyodai kutoka kwa Jeshi la Polisi kuwa ni suruali za vitambaa na jeans saba, simu tatu, redio za biashara ambavyo kwa pamoja alidai vina thamani ya Sh. milioni 1.66.

"Vitu vingine niliambiwa nimpigie simu kamanda wa mkoa nitapewa. Kwa hiyo, sijajua nini kinachoendelea," Sadiki alidai.

Mfanyabiashara huyo alidai kuwa akiwa gerezani, alikutana na mahabusi wengine waliodai kubambikwa kesi za mauaji na Jeshi la Polisi mkoani Tabora.

"Unaweza ukawa umekamatwa kwa kosa la kuvunja na kuiba na ukawa katika harakati zako, ukakamatwa na mali zako au kupekuliwa nyumbani, unanyang'anywa vitu vinapelekwa polisi, vinakuwa vyao na unapewa kesi ya mauaji. Hili naomba walifuatilie hata huko nilikotoka nimeacha wengine wana kesi za kubambikwa za mauaji," Sadiki alidai.

# Marekani yawamwagia wanawake bil. 1.1/-

INATOKA UK. 2

kampeni, jinsi ya kuandaa ujumbe na kutumia sera.

Aidha, alisema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, kaulimbiu ya 'usawa bora' inaendana na mazingira ya Tanzania kwa sasa wakati ikiongeza kasi ya maendeleo yake kuelekea uchumi wa kati.

"Nchi zisipotilia mkazo kujenga uwezo wa wasichana na wanawake zinasahau kwamba wanawake waliojengewa uwezo wana uwezo wa kuleta mageuzi kwenye jamii," alisema.

Alisema ukosefu wa elimu na afya ni vikwazo ambavyo vinasababisha wasichana na wanawake washindwe kuishi maisha ya kujitosheleza na kuchangia kutokuwapo kwa usawa katika jamii.

Dk. Patterson alisema changamoto kubwa kwa wanawake wengi ni kukosa nguvu, ushawishi na sauti ya kufanya uamuzi muhimu unaohusu maisha yao na kutenda kwa uhuru bila kuogopa.

Aidha, alisema wanawake wamekuwa na uwakilishi hafifu kwenye michakato ya kisiasa na uchaguzi na changamoto hiyo haiko kwa Tanzania pekee.

Balozi huyo alisema hali hiyo inaonyesha kwa kiasi kikubwa jinsi wanawake wanavyotengwa kwenye nafasi nyingi za juu za kufanya maamuzi kwenye serikali kuu na vyama vya siasa.

Dk. Patterson alisema kauli ya uwezeshaji wanawake imetumika zaidi duniani, hivyo kuna haja ya kuwepo kwa mabadiliko ya kweli ambayo yataleta usawa katika fursa na kuondoa mila zinazowaondolea thamani.

Naye Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na Masuala ya Wanawake, (UN Women) Hodan Addiu, alisema wanawasaidia wanawake kupata uongozi katika masuala ya siasa na kushiriki uchaguzi.

Alisema wameshirikiana na serikali ya Marekani katika kuwainua wanawake kupitia mradi huo wa awamu ya pili, washiriki kupata uongozi kwa kuwapatia mafunzo ambayo yatawajengea uwezo.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda, alisema kabla ya kuchaguliwa kuwa mbunge alipatiwa mafunzo hayo ambayo yamemsaidia kujiamini na kuweza kuuliza maswali bungeni.

Aliwashauri wanawake wajitokeze kwa wingi ili wapatiwe mafunzo hayo ambayo yatawasaidia kugombea nafasi za juu za uongozi wanapoelekea katika uchaguzi.

## HABARI KITAIFA

# Wakulima waliangukia Bunge malipo korosho

**Abdallah Bakari,** MTWARA

WAKULIMA wa korosho mkoani Mtwara, wameliomba Bunge kuingilia kati ucheleweshwaji wa malipo yao kwa kuishinikiza serikali kutekeleza kwa vitendo ahadi inazozitoa kwa kile walichokidai kuwa wamechoshwa na matamko yanayokosa utekelezaji.

Kwa nyakati tofauti, wakizungumza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji katika wilaya za Tandahimba na Newala mkoani hapo jana, wakulima hao walisema licha ya serikali kutoa maagizo kwa watendaji kuwalipa wakulima fedha zao, utekelezaji wake umekuwa ukisuasua.

Walisema iwapo Bunge litaingilia kati kwa kuisimamia serikali kuhakikisha wakulima wa korosho wanalipwa fedha zao kwa wakati, itasaidia kuwatatulia shida walizo nazo zikiwamo madeni yanayotokana na vibarua na maandalizi ya msimu ujao.

Wakulima wa Tandahimba ndio waliofungua pazia ya kuonyesha kutoridhishwa na mwenendo wa malipo ya zao lao hilo mapema, wakati wa salamu, kwa kujibu hoi badala ya hai na mbaya badala ya safi.

"Korosho haiii, hoiiii? Alihoji Mbunge Sikudhani Chilambo (Viti Maalum -CCM) ikiwa ni sehemu ya salamu na kujibiwa "hoiiiii". "Haiiii hoiiii?," Alihoji tena mithili ya mtu anayetaka uhakika wa jibu na kisha kujibiwa kwa sauti ya juu "hoiiiiiiiiiii" na baadaye aliendelea "korosho safiiii?" Akajibiwa "mbayaaaa".

Baada ya salamu hizo zilizoashiria mambo kutokuwa mzuri, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Christina Ishengoma, alitoa nafasi kwa wakulima kuelezea kero zao na ndipo walipoiomba Bunge kuingilia kati suala hilo.

"Tandahimba tuna tatizo la fedha. Watu hawajalipwa fedha zao. Tunataka fedha zetu, wakulima walipwe fedha zao...fedha za maendeleo hatupati na hata za kwake asipate?" Alihoji Onja Masaninga, mkulima wa Tandahimba na kuongeza kuwa:

"Tatizo liko wapi kama Rais (John Pombe Magufuli) aliagiza tulipwe, Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) aliagiza tulipwe, lakini bado wakulima hatulipwi. Kwa kuwa Kamati ya Bunge imefika, tunaomba Bunge lisimamie wakulima tulipwe fedha zetu."

Mwenyekíti wa Halmashauri hiyo, Namkulya, alisema mbali na wakulima kutolipwa fedha zao pia kukosekana kwa ushuru kumeiathiri halmashauri hiyo kwa asilimia 100.

"Asiliamia 95 ya mapato yetu ya ndani yanategemea korosho, asilimia tano inategemea mnyororo wa thamani ya korosho, hivyo asilimia 100 tunategemea korosho. Hapa tulipo hakuna hata mradi mmoja unaotekelezwa kwa fedha za ndani. Tunaomba kamati na mheshimiwa waziri mliangalie hili, halmashauri tulipwe ushuru wetu unaotokana korosho," alisema na kuongeza:

"Ucheleweshaji wa malipo ya korosho unaweza kusababisha kuanguka zaidi katika uzalishaji kwa msimu ujao.

Msimu wa 2017/18 tulizalisha tani 740,000 kutokana na kukosekana kwa pembejeo za ruzuku. Mfuko wa salfa uliuzwa kwa Sh. 70,000 kutoka Sh. 14,000 ya bei ya ruzuku, wakulima wengi walishindwa kumudu na hatimaye uzalishaji ukaanguka na kufikia nusu yake tani 38,000."

Alibainisha kuwa ucheleweshaji wa malipo na kukosekana kwa viuatilifu vinaweza kuchangia kuporomoka zaidi kwa zao hilo, hivyo kuomba mamlaka husika kuchukua jitihada za makusudi kunusuru zao hilo.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akishiriki kuteketeza nyavu haramu zilizokamatwa katika uvuvi haramu Bahari ya Hindi eneo la Moa wilayani Mkinga, mkoani Tanga juzi. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Mark Yona na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi na Kupambana na Uvuvi Haramu, Nchama Marwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC apiga marufuku faini wajawazito

**Na George Tarimo,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, amepiga marufuku wenyeviti wa vijiji na kata kuwatoza wanawake faini ya Sh. 50,000 kwa kile kinachodaiwa wameshindwa kuhudhuria kliniki wakiwa wajawazito na badala yake faini hizo zielekezwe kwa wanaume.

Hapi alisema juzi, kuwa katika ziara yake aliyoifanya mwishoni mwa mwaka jana na kuipa jina la 'Iringa Mpya', moja ya kero alizokutana nazo ni wanawake kutozwa faini hiyo ambayo wengi wao wanashindwa na kujikuta wanazalia nyumbani.

"Nilifanya mikutano mingi sana, kila kona ni tozo ya Sh. 50,000. Nikajiuliza ni ya nini, lakini niliambiwa baadhi ya vituo vyetu vya afya na zahanati walikubaliana kutoza wanawake fedha hiyo kwa sababu hawakuhudhuria kliniki. Walikuwa na nia njema, lakini kwa kuwa kosa si lao na wengine wanaweza kukimbia hospitali basi faini hizo zielekezwe kwa wanaume au wenza wao wanaowapa mimba," alisema Hapi.

Hapi aliwataka wanaume kujenga mazoea ya kuwasaidia wake zao pindi wanapokuwa wajawazito kwa kuwapeleka katika vituo vya afya ili kupatiwa huduma za awali, huku akiwaagiza viongozi wa halmashauri za vijiji kuanza kuwatoza fedha wanaume watakaoshindwa kuwasaidia wenza wao kipindi cha ujauzito.

Alisema mawasiliano yanayolenga kubadili tabia yanahitajika kwa kina na kwa kiwango kikubwa ili wananchi kutumia huduma za afya.

"Hizi juhudi kama hazitaenda sambamba na mabadiliko ya tabia hatuwezi kufanikiwa. Tunahitaji wananchi watumie hizi huduma za afya na ndani ya mkoa wa Iringa tunalo tatizo kubwa wanawake wengi wanaopata ujauzito hawaendi kliniki. Nitoe wito faini hizi zielekezwe kwa kina baba kuanzia sasa," alisema.

"Badala ya kuhangaika na kinamama tushughulike na kinababa waliowapa ujauzito hawa kinamama ili wahakikishe wenza wao wanaenda kliniki sasa. Watendaji wote, kata zote na halmashauri zote ndani ya mkoa huu faini hizi sasa tuanze kuwatwanga kinababa," aliongeza.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Jukwaa la Mawasiliano ya Afya kwa Watu Wazima lijulikanalo kama Naweza, imezindua mpango wa kusaidia kufikisha ujumbe wa mabadiliko ya tabia za jamii husasani wanaume kuwasaidia wake zao wanapopata ujauzito.

Mtaalamu wa afya ya uzazi na mtoto katika Wizara ya Afya, Martha Shakinyau, alisema serikali iko katika mpango wa kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga hadi kufikia 292 katika vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020.

Shakinyau alisema kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na wizara kupitia Kitengo cha Afya ya Uzazi na Mtoto, vifo vitokanavyo na uzazi ni 556 kwa mwaka katika vizazi hai 100,000, jambo linalotishia usalama wa maisha ya wanawake na watoto nchini.

# Aliyemwokoa nyangumi aahidiwa kulipwa fidia

**Na Boniface Gideon,** MKINGA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema itamlipa fidia Puyuyu Abdalah, mkazi wa kata ya Moa wilayani Mkinga, baada ya kumwokoa samaki aina ya nyangumi aliyenaswa kwenye nyavu zake alizokuwa amezitega baharini Oktoba 2, mwaka jana.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wavuvi wa wilaya ya Mkinga.

Alisema mwananchi huyo alipoona nyangumi amenaswa kwenye nyavu zake, alifanya uungwana kwa kutoa taarifa serikalini ndipo wataalamu wa wizara walipofika na kumtoa.

Mpina alisema baada ya wataalamu hao kufika, walimwomba mwananchi huyo awaruhusu kuchanwa nyavu ili samaki huyo adimu aendelee na safari zake na alikubali kupata hasara ya nyavu zake saba zilizounganishwa.

Alisema mwananchi huyo atalipwa fedha za thamani ya nyavu zote kutokana na uzalendo wake mkubwa kwa taifa.

"Naomba achague mwenyewe kama atataka alipwe nyavu sawa au kama atataka alipwe pesa yote sawa, ataangalia mwenyewe," alisema.

Alipohojiwa na Nipashe, mwananchi huyo alisema nyavu hizo kila moja ina thamani ya Sh. 550,000 hivyo zote zina thamani ya Sh. 3,850,000 na kuongeza kuwa endapo serikali itamlipa itakuwa imemwokoa kwa kuwa hivi sasa anaishi katika mazingira magumu kutokana na kutokuwa na nyavu.

"Sasa hivi nahangaika hangaika tu, nadandia kwenye vyavu za wenzangu, hivyo naomba serikali ifanye haraka ili nipate kujikwamua kimaisha kwa kuwa uvuvi kwangu ndilo tegemeo la maisha yangu," alisema.



Mfanyabiashara Merrysiana Shija, kutoka Soko la Ndembezi Shinyanga Mjini, akielezea namna wanavyofanyiwa matukio ya ukatili wa kijinsia kwenye masoko ikiwamo na kutukanwa matusi ya nguoni. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Ruaha kuanzisha utalii wa boti

**Novatus Makunga,** ARUSHA

USAFIRI wa boti unatarajia kutumika katika Mto Ruaha ikiwa ni kivutio kipya cha utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, mkoani Iringa, kuanzia mwakani.

Tayari aina nyingine ya utalii wa kuruka kwa kutumia puto ulishaanza katika hifadhi hiyo mwaka 2018. Utalii wa kuruka kwa puto umekuwa ukitumika zaidi kwa miaka mingi katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, ukanda wa kaskazini.

Meneja Uhusiano wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Paschal Shelutete, aliiambia Nipashe kuwa hatua hiyo imelenga kuongeza na kukuza sekta ya utalii katika ukanda wa kusini.

Shelutete alisema kuwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ndiyo mbuga kubwa kuliko zote Afrika na ina vivutio vingi ambavyo baadhi yake havipatikani katika maeneo mengine ya dunia vikiwamo vivutio vya asili na utamaduni.

"Huu ni mpango kabambe wa Tanapa kufungua utalii katika ukanda wa kusini ambayo ina vivutio lukuki," alisema Shelutete.

Shelutete alisema pia shirika hilo tayari limehamasisha utalii wa kuruka angani kwa kutumia puto (balloon) katika hifadhi hiyo ya Ruaha.

Shelutete alisema kuwa Tanapa imeamua kuhamasisha wawekezaji kuwekeza kwenye utalii wa kusafiri kwa boti na kuruka kwa puto katika Hifadhi ya Ruaha.

Alisema utalii huo utahusika na usafirishaji wa watalii ndani ya hifadhi hiyo kutoka eneo moja kwenda lingine na utatoa fursa kubwa kwa watalii kutumia saa chache na kutembelea maeneo mapana zaidi na pia kuona wanyama wengi zaidi kwa muda mfupi.

"Utalii huu utawapa urahisi zaidi watalii kuona vivutio vingi na watasafiri kwa urahisi zaidi kuliko wanavyotumia usafiri wa magari," alisema.

Idadi ya watalii waliokwenda kutembelea vivutio vya watalii nchini iliongezeka kutoka watalii 1,284,279 mwaka 2016 hadi kufikia 1,327,143 mwaka 2017.

Katika kipindi hicho mapato ya serikali yanayotokana na utalii yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 2.1, mwaka 2016, hadi dola bilioni 2.2 mwaka 2017.

# DTB yazindua huduma kufikia wateja wa mbali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya DTB-Tanzania jana, imezindua huduma tatu za kuwafikia wateja walio mbali na matawi na kupunguza gharama za kupata huduma za kibenki kwa wateja wake.

Huduma hizo ni pamoja na Prepaid Card, DTB Wakala na Merchant Payment devices (POS).

Taarifa iliyotolewa na benki hiyo, ilisema kadi hizi za Pre-Paid ambazo zipo kwenye mfumo wa MasterCard, zina uwezo wa kubeba fedha aina 10 zinazotambulika kimataifa tofauti na shilingi ya Tanzania ambayo ni fedha namba moja.

"Kadi hizi zinafaa kwa wafanyabiashara wanaosafiri nje ya nchi kwa matibabu, wanafunzi wanaosoma nje ya nchi na watalii. Fedha hizi ni pamoja na Dola za Kimarekani, Yuro ya bara la Ulaya, Paundi ya Uingereza, Dirham ya Ufalme za Kiarabu, Rupee ya India, Randi ya Afrika Kusini, Yuan ya Uchina, Dola ya Canada na Shilingi za Kenya na Uganda," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, ilisema kadi hizo zipo kwenye teknolojia ya hali ya juu ili kuimarisha usalama kwa wateja na haziwezi kughushiwa kwa namna yoyote.

Akizungumza na wageni waalikwa katika hafla ya uzinduzi, Mwenyekiti wa Bodi ya DTB - Tanzania, Abdul Samji, alisema, dhamira ya benki ni kuboresha huduma kwa wateja kwa kuwekeza kwenye teknolojia. "Nina furaha kwamba kwa mara nyingine tunawaletea huduma salama, rahisi na yenye thamani kwa pesa za wateja wetu."

"Kwa kuzindua huduma kupitia mawakala, wateja wetu watapata huduma za kibenki moja kwa moja kupitia mawakala 110 ambao wamesambaa nchi nzima. Huduma zinazopatikana kwa kupitia mawakala wetu ni kuweka fedha, kutoa pesa na kuangalia taarifa fupi za miamala.

Huduma za kibenki kupitia mawakala ni mkakati mahususi wa kuongeza ufanisi kiuchumi kwa kufikia Watanzania waliopo katika maeneo ambayo hakuna huduma za kibenki zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wote.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa huduma kupitia mawakala zinakuwa muhimu hasa katika sehemu ambazo benki haziwezi kuweka matawi kulingana na uwekezaji unaohitajika.

Merchant Point of Sales (POS) Machines, ambazo zinatumia Visa na MasterCard ni mahusus kwa malipo kwenye maduka makubwa (Supermarkets) hoteli na migahawa na pia maduka ya kawaida. Machine hizo hutumika kufanya malipo moja kwa moja toka kwenye akaunti ya mteja badala ya kutembea na pesa taslimu. Merchant Point of Sales (POS) zinapunguza kwa kiasi kikubwa gharama na madhara ya kutembea na pesa taslimu.

DTB-Tanzania kwa sasa ina matawi 28 nchini, 14 kati ya hayo yakiwa jijini Dar es Salaam.

DTB-Tanzania ni kampuni tanzu ya kampuni ya DTB (DTB Group) inayoendesha shughuli za kibiashara katika ukanda wa Afrika Mashariki nchini Kenya, Uganda na Burundi. DTB Tanzania pia ni kampuni tanzu ya Mfuko wa Aga Khan wa Maendeleo ya Kiuchumi (The Aga Khan Fund for Economic Development - AKFED) ambayo ni tawi la Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (Aga Khan Development Network -AKDN).

# Wanawake sokoni walia kunyanyaswa kijinsia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAWAKE wanaofanyabiashara ya kuuza bidhaa mbalimbali kwenye masoko ya Shinyanga Mjini, wamelalamika kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye maeneo hayo, ikiwamo kutolewa lugha chafu za kuwadhalilisha viungo vya maumbile yao.

Walitoa kilio hicho jana kwenye uzinduzi wa mradi wa kuzuia ukatili wa kijinsia kwenye masoko ya Shinyanga Mjini, utakaotekelezwa na Shirika la Agape la mkoani hapa, ambalo linajishughulisha na shughuli ya kupinga ukatili kwa watoto na wanawake, utakaodumu mwaka mmoja.

Mmoja wa wanawake hao, Merysiana Shija, mfanyabiashara katika Soko la Ndembezi, alisema wamekuwa wakikumbana na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo kutolewa lugha chafu kutoka kwa wafanyabiashara wenzao wa kiume na baadhi ya wateja pamoja na kudhulumiwa pesa.

"Nalipongeza sana Shirika hili la Agape kwa kuzindua mradi huu wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwenye masoko yetu ya Shinyanga mjini, sababu imekuwa ni kero kwetu sisi wanafanyabiashara wanawake, tunatukanwa matusi ya nguoni pamoja na kudhulumiwa kwa kutolipwa pesa zetu na baadhi ya wateja wa kiume," alisema Shija.

"Mfano kwenye biashara yangu ya awali ya mamalishe niliachana nayo baada ya mtaji kukatika, nilikuwa nikilisha wachimba msingi wa barabara kwa tenda, lakini baada ya kazi yao kuisha waligoma kunilipa huku nikiambulia na matusi juu ya nguoni, nikaamua kuanza upya biashara nyingine," aliongeza.

Baadhi ya wenyeviti wa masoko ya Shinyanga mjini akiwamo Hassani Baruti wa Nguzo Nane na Tracey Leonard wa Ndembezi, kwa nyakati tofauti walikiri kuwapo na matukio hayo ya ukatili wa kijinsia kwa wafanyabiashara wanawake, mengine wamekuwa wakiyatatua kupitia vikao vya sokoni.

Naye Ofisa mradi huo wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwenye masoko ya Shinyanga mjini, Mustapha Isabuda, kutoka Shirika hilo la Agape, alisema wameuanzisha baada ya kufanya utafiti na kugundua wafanyabiashara wengi wanawake wanafanyiwa ukatili na kutokujua wapi pa kupata haki zao.

Kwa upande wake Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Shinyanga, Bestina Gunje akimwakilisha Mkurugenzi wa manispaa hiyo, Geofrey Mwangulumbi, aliwataka wafanyabiashara wanawake wasiwe wanakaa kimya pale wanapofanyiwa ukatili kwa kutoa taarifa ili wasaidiwe kupata haki zao.

# Kamati ya Bunge yabaini madudu mradi wa maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUMERU

MRADI wa maji wa Loovilukuny uliopo Halmashauri ya Arusha umeshindwa kukamilika kwa zaidi ya miaka sita, baada ya serikali kushindwa kulipa fedha za madai ya malipo kwa wakati.

Kucheleweshwa kulipwa kwa fedha hizo, kumesababisha gharama za mradi huo kuongezeka kutoka Sh. milioni 777 za awali hadi kufikia Sh. bilioni 1.35.

Akizungumza kwa niaba ya makandarasi wenzake mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, iliyotembelea mradi wa Loovilukuny mmoja kati ya miradi 10 iliyopo wilayani Arumeru jana, mkandarasi Samuel Rugemalila, alisema ucheleweshwaji wa fedha unasababisha miradi ya maji kuchelewa kumalizika kwa wakati.

Alisema mradi wa Loovilukuny umechelewa kukamilika kwa zaidi ya miaka sita sasa.

Alisema hali hiyo imesababisha gharama za mradi kupanda kutoka Sh. milioni 777 za awali hadi hadi kufikia Sh. bilioni 1.35.

Alisema mradi huo ulianza mwaka 2013, licha ya changamoto alizokumbana nazo, hadi sasa umefikia asilimia 99 na ameshalipwa Sh. milioni 902, lakini bado anadai fedha nyingine.

"Si katika mradi huu tu, nimefanya kazi Babati nikakamilisha mradi wa Sh. bilioni 1.2 kwa wakati na Monduli mradi mmoja wa miezi sita, lakini hadi sasa sijalipwa fedha zangu licha ya kuwasilisha hati za madai wizarani," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mahmoud Mgimwa, alisema ni vyema serikali ikaharakisha ulipwaji wa nyaraka za madai kwa makandarasi zinazowafikia kwa wakati ili kuokoa gharama.

"Sasa mmejionea wenyewe wajumbe wenzangu kama mradi umechelewa kwa miaka sita gharama za mradi zimepanda hadi Sh. bilioni 1.35 kwa sababu ya ucheleweshwaji usio wa lazima, msicheleweshe miradi ya maendeleo hususan ya maji," alisema.

Kwa upande wao uongozi wa Wilaya ya Arumeru, ulisema licha ya serikali kuchelewesha fedha za miradi, umekuwa ukizungumza na viwanda vinavyozalisha mabomba na kuwakopesha makandarasi, ili miradi ya maji isikwame kwa kuwa wananchi wanahitaji maji.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga (wapili kulia) na baadhi ya watumishi wa halmashauri ya wilaya hiyo, wakifurahia picha ya jengo jipya la makao makuu ya halmashauri hiyo juzi, litakalojengwa Kata ya Dongobesh. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mizengo Pinda kutembelea majimbo saba ya CCM

**Na Mwandishi Wetu,** KITETO

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Manyara, ameanza ziara ya siku nane kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM na kufanya vikao vya ndani katika majimbo yote saba yanaongozwa na chama hicho.

Akiwasili wilayani Kiteto, Pinda alipokelewa na viongozi wa serikali na CCM katika Kata ya Dosidosi akitokea jijini Dodoma juzi.

Katika mapokezi hayo, alisema Watanzania wote wanapaswa kumuunga mkono Rais Magufuli ambaye anafanikisha maendeleo katika sekta mbalimbali bila ubaguzi wa vyama, itikadi, udini wala ukabila.

Alisema ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais Magufuli wananchi wanapaswa kuchangia miradi ya maendeleo ili kuleta tija kwa jamii.

Pinda alisema lengo kubwa la ziara yake mkoani humo ni kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM kwenye majimbo yote saba ambayo hivi sasa yanaongozwa na CCM. Katibu wa CCM, Wilaya ya Simanjiro, Ally Kidunda, alisema mlezi huyo wa CCM baada ya kutokea wilayani Kiteto atapokelewa kijiji cha Londrekes, kilichopo Kata ya Kitwai, ambapo ni mpakani mwa Wilaya ya Simanjiro na Kiteto.

Alisema baada ya kuwasili Londrekes, Pinda atafanya kikao cha ndani na viongozi na wanachama wa CCM mjini Orkesumet, na atawapokea wanachama wapya kijiji cha Okutu na kisha ataweka jiwe la msingi la CCM tawi la Nakweni.

"Baada ya hapo msafara wake utaelekea mji mdogo wa Mirerani, ambapo ataongea nao kwenye mkutano wa ndani utakaofanyika ukumbi wa Songambele," alisema.

Kwa mujibu wa Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Manyara, Jacob Siay, ziara hiyo ya Pinda itakuwa ya siku nane.

Alisema Pinda atatembelea majimbo saba ya Kiteto, Simanjiro, Babati Vijijini, Babati Mjini, Hanang' Mbulu Vijijini na Mbulu Mjini.

# Mirerani watekeleza miradi ya bil. 1.7/-

**Na Mwandishi Wetu,** MIRERANI

MAMLAKA ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, imefanikisha miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.7 katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wao.

Mwenyekiti wa mamlaka hiyo, Adam Kobelo, aliyasema hayo kwenye kikao maalum cha baraza la mamlaka hiyo.

Alisema miradi hiyo imejikita kwenye sekta mbalimbali ikiwamo 14, mikubwa ya elimu, afya, maji, ardhi, barabara na mengineyo.

Alisema baadhi ya miradi hiyo imefanikishwa na Serikali Kuu, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, taasisi binafsi, kampuni binafsi na watu binafsi wakiwamo wafanyabiashara wa madini ya tanzanite.

"Tulikaa vikao sisi kama viongozi tukachakata tukawafuata wadau wa maendeleo kisha wakachangia maendeleo nasi tunapaswa kupongezwa kwenye hilo," alisema.

Alitaja baadhi ya miradi hiyo ni madarasa, jengo la utawala na maabara ya Shule ya Sekondari Songambele na madarasa matano ya Shule ya Msingi Songambele. Alitaja miradi mingine ni jengo la mama na mtoto Kituo cha Afya Mirerani, kisima cha maji, jengo la CTC na jengo la kuhifadhi maiti lililopo hatua ya kukamilika.

"Miradi mingine ni madarasa mawili ya Shule ya Msingi Jitegemee, kisima cha maji Shule ya Msingi Songambele, kiwanda cha ngozi, mashine ya kiwatesi na upimaji wa viwanja," alisema.

Alisema bado wana changamoto ya uhaba wa madarasa, ukosefu wa nyumba za walimu, umaliziaji maabara ya Shule ya Sekondari Mirerani Benjamin Mkapa na samani za Shule ya Sekondari Songambele.

Alisema anatarajia wananchi watatambua juhudi zao za maendeleo na ili kuwaunga mkono watawachagua tena viongozi hao kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Oktoba mwaka huu.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Simanjiro, Awadhi Omary, aliwapongeza viongozi hao kwa kufanikisha miradi hiyo ya maendeleo kwa wananchi.

Alisema kutokana na kuchapa kazi kwa bidii na mafanikio hadi kufanikisha maendeleo ana imani wananchi watawachagua tena kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.







Mafundi wakibomoa nyumba ili kupisha ujenzi wa reli ya kisasa ya Standard Gauge katika eneo la Ukonga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Hospitali ya KCMC yatangaza uhaba wahudumu wa afya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya KCMC mkoani Kilimanjaro inakabiliwa na upungufu wa wauguzi 498 katika hatua inayodaiwa kusababisha wahudumu kuelemewa na kazi na hivyo kuathiri utoaji huduma hospitalini hapo.

Hayo yamo katika ripoti ya Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo na Katibu wa Shirika la Msamaria Mwema Tanzania (GSF), Dk. Gileard Masenga.

Masenga alikuwa akizungumza na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo kuhusu mafanikio na changamoto zinazoikabili hospitali hiyo ya rufani ya mikoa ya kanda ya kaskazini.

KCMC ni hospitali inayomilikiwa na Kanisa la KKKT na inasimamiwa na Shirika la Msamaria Mwema. Shirika hilo limesaini mkataba maalumu (MoU) kati yake na serikali, ambapo serikali inagharamia matumizi ya kawaida na shirika linagharamia mali zake ambazo hazihamishiki kama majengo na ardhi.

"Kwa sasa tuna wauguzi 198 tu, lakini kwa uhalisia tulitakiwa kuwa na wauguzi 696. Aidha, bado hospitali ina upungufu wa madaktari bingwa na kwa sasa kuna madaktari bingwa 48 tu, ambapo kulitakiwa kuwa na madaktari bingwa 100," alisema.

Kuhusu utoaji wa huduma kwa wagonjwa wanaolazwa hospitalini hapo, Dk. Masenga ameeleza kuwa kwa sasa hospitali ina jumla ya vitanda 639.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, idadi ya wagonjwa huwa inaongezeka na kusababisha wagonjwa kulala katika korido.

Kutokana na hali hiyo, walilazimika kufanya upanuzi wa kitengo cha wagonjwa wa nje na wagonjwa wa ndani. Idadi ya wagonjwa wa nje ni kati ya wagonjwa 600, mpaka 800 kwa sasa.

Kwa sasa hospitali inapokea wagonjwa kati ya 36,470 kwa mwezi, ambapo asilimia 79.7 ya wagonjwa wote wanaohudumiwa katika Hospitali ya KCMC wanatoka kwenye mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, na Singida.

# Kampuni tatu zajitokeza kupima ardhi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imeziteua kampuni tatu zinazojihusisha na shughuli za upimaji ardhi nchini kikiwamo Chuo cha Ardhi Morogoro, kuanza upimaji wa ardhi katika kata tano za Manispaa ya Moshi ili kumaliza migogoro na kurahisisha urasimishaji wa makazi holela.

Kampuni mbili zilizoungana na chuo hicho kutekeleza agizo la Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ni Land Survey Consult Ltd na AG Analysis, zote za Dar es Salaam.

Jana, Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, alithibitisha kuanza kazi kwa wapimaji hao katika baadhi ya mitaa katika kata tano za Longuo, Rau, Njoro, Msaranga na Ng'ambo.

"Ni kweli hizo kampuni zinapima huko mitaani hivi sasa, tunaomba wananchi wetu wawaunge mkono kwa sababu ni kwa faida yao. Watalaamu wa kampuni hizi watakiwa kushirikiana na Idara ya Ardhi na Mipango Miji kuhakikisha wananchi hasa wenye kipato cha chini wanarasimishwa," alisema.

Mara kadhaa Waziri Lukuvi amekuwa akielekeza kuwa mikakati ya serikali ni kuhakikisha ardhi yote ya Tanzania inapangwa, kupimwa na kumilikishwa kisheria.

Wiki iliyopita, Waziri Lukuvi wakati anazindua mpango wa kutambua na kusajili kila kipande cha ardhi mijini, alisema serikali imekuja na mpango huo wenye lengo la kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kwa wananchi na kuwawezesha kushiriki katika maendeleo.

Alisema mpango huo ambao unategemewa kutekelezwa katika mitaa ambayo haijapimwa na haipo katika zoezi la urasimishaji katika halmashauri zote na mijini, hautahusisha wakazi waliopo katika maeneo hatarishi ikiwamo mabondeni na maeneo yaliyopita gesi.

Pamoja na mambo mengine, ameeleza kuwa ili wananchi waweze kushiriki maendeleo hayo, usalama wa miliki ya ardhi yao ni suala muhimu, ambapo katika hilo leseni za makazi cha kutumia ardhi mijini hutolewa kama hatua za awali za umilikishaji katika maeneo yaliyojengwa kiholela wakati taratibu za mipango mingine juu ya eneo husika zinaendelea.

"Mpango huu wa kutambua kila kipande cha ardhi mijini ambao unaanzia Mkoa wa Dar es Salaam utatekelezwa nchi nzima, utekelezaji wake utagharamiwa na serikali kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji," alisema Lukuvi.

# Mwanafunzi akatisha masomo kwa ujauzito

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MWANAFUNZI mmoja wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Matadi iliyoko Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, amekatisha ndoto yake ya kuendelea na masomo, baada ya kufukuzwa shule kutokana na kupata ujauzito.

Mtuhumiwa anayesadikiwa kutenda kosa hilo dhidi ya mwanafunzi huyo, hajakamatwa mpaka sasa na hajulikani alipo.

Mkuu wa Shule hiyo, Betram Ndumba, amethibitisha kuwa mwanafunzi huyo ameshakatisha masomo yake tangu mwezi huu.

"Ni kweli toka Januari hadi Machi, kuna mwanafunzi mmoja wa kidato cha nne amepata ujauzito na mwaka jana pia mwingine alikatisha masomo yake vivyo hivyo. Tunajitahidi kutoa elimu kwa wanafunzi na wazazi wanapokuja lakini bado suala hilo ni changamoto," alisema Ndumba.

Mkuu huyo wa shule ameeleza kwamba tayari suala hilo limesharipotiwa katika Kituo Kikuu cha Polisi Sanya Juu kwa ajili ya hatua zaidi.

Hali ya mimba za utotoni kwa wanafunzi wa shule za sekondari katika Wilaya ya Siha, inadaiwa kuchangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo vishawishi na kurubuniwa kwa wasichana wadogo kutokana na umbali wa shule hizo na makazi ya watu.

Diwani wa Kata ya Ndumeti, Jackson Rabo, alipoulizwa kuhusiana na changamoto hiyo amekiri changamoto kama hizo kujitokeza katika baadhi ya maeneo, ingawa wameendelea kuchukua hatua kali na sasa wanaongeza nguvu kudhibiti kabisa hali hiyo.

Tatizo hilo la ujauzito kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika wilaya hiyo limeendelea kuumiza vichwa viongozi wa ngazi ya serikali, wazazi na wadau wa elimu hasa baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuagiza kusakwa kwa watu wote waliowapa mimba wanafunzi na kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

Februari 25, mwaka huu, Majaliwa akiwa katika wilaya hiyo alisema katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba mwaka jana, jumla ya wanafunzi wa kike 57, walikatishwa masomo baada ya kupata mimba na hadi sasa kesi zilizofunguliwa ni sita pekee.

# ama

ALHAMISI MACHI 21, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 17

**Wazazi wavamia shule kwa vyakula vilivyooza**



Ukurasa 16

Baa la njaa kwa maelfu ya wafugaji, minong'ono ya vifo



Ukurasa 14

**Siku ya Kufurahi Duniani...**



# Aliyesimama kwa vidole maishani, mara ya kwanza atumia nyayo zake

Ukurasa 14

# Siku ya Kufurahi Duniani...

JANA ilikuwa Siku ya Kimataifa ya Kufurahi. Inaelezwa kitaalamu, furaha inafanyika kwa njia tano.

Mtaalamu Profesa Laurie Santos wa Chuo Kikuu cha Yale, Marekani, anasema:"Sayansi imedhihirisha kwamba kuwa na furaha inahitaji jitihada za kusudi. Sio rahisi na huchukua muda."

Anataja njia tano za kufikia furaha: Mosi, ni kutengeneza orodha ya kuwa na shukrani, akiwahimiza zaidi wanafunzi waandike mambo wanayoshukuru maishani mwao kila siku.

Pili, ni kulala muda mrefu kwa wastani wa saa nane kila siku, kwa kuwa kunapunguza msongo wa mawazo.

Tatu, mtu ajipe muda kutafakari angalau dakika 10 kila siku, jambo ambalo profesa huyo anasema binafsi imemsaidia sana.

Nne, kupata muda wa kujiliwaza na kuzungumza ma marafiki, jambo linalokaribisha furaha na mwisho, la tano ni kupunguza uhusiano wa mitandao wa kijamii, badala yake kuwekeza zaidi katika uhusiano halisi. **BBC.**



Profesa Laurie Santos, akitabasamu. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

UPASUAJI WA KIHISTORIA MOI

# Aliyetumia vidole, mara ya kwanza atumia nyayo zake

- Alitegemea mchuchumio kila mahali

**Na Mary Geofrey**

UBORESHAJI wa huduma za matibabu katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), umeweza kubadili maisha ya binti ambaye kwa miaka 20, hajawahi kukanyaga ardhi kwa kutumia miguu.

Kwa mwaka mmoja wa matibabu aliyopatiwa MOI na madaktari bingwa na vifaa vya kisasa vilivyopo, ameweza kutembea akitumia nyayo zake, jambo ambalo hakuwahi kulifikiria kutokea.

Doris Martin (21), mkazi wa mkoa wa Kagera, alifunga safari mwaka jana kufika jijini Dar es Salaam, akiongozana na mama yake mzazi, Philemina Martin.

Anasema, alianza kuugua tangu utotoni na hakuweza kutembea kwa kukanyaga nyayo zake chini, bali alitumia vidole vya miguu kusimama.

Doris anasimulia kwamba baada ya kukaa kimya kwa miaka mingi, alishindwa kusimama peke yake, hivyo kuanza kutumia viatu vya mchuchumio.

"Nilikuwa siwezi kabisa kusimama mwenyewe, bila ya kutumia viatu vya mchuchumio. Nilipokuja MOI mwaka jana, wakaniambia nina tatizo la miguu na wakaanza kunipatia matibabu," anasema Doris.

Anaeleza kwamba, walianza kumfanyia upasuaji mguu wa kwanza kwa ajili ya kushusha baadhi ya mifupa, ili iweze kuzifanya nyayo zilingane na aweze kukanyaga chini.

Doris anasema, baada ya miezi mitatu walimfanyia upasuji mguu wa pili na sasa wamemfunga vyuma na kumvalisha viatu vya raba, vinavyomfanya akanyage chini bila ya shida.

"Namshukuru Mungu na madaktari wote wa MOI, kwa kuniwezesha kukanyaga chini peke yangu kwa mara ya kwanza kwenye maisha yangu. Awali nilikuwa siwezi kabisa na sijawahi kukanyaga chini," anasema Doris.



Doris Martin, akiwa na mama yake, Philomena Martin.

Anaongeza kuwa, tukio hilo la kuanza kukanyaga chini kwa mara ya kwanza, lilimshtua mama yake mzazi na hata akapoteza fahamu kwa muda kutokana na mshtuko wa tukio hilo.

Mwanamke huyo anafafanua kuwa, hadi sasa anaendelea na wamemwahidi, baadaye wataangalia namna ya kuanza kumfanyia matibabu ya mgongo na shingo, ambayo kwa sasa inamsumbua.

"Madaktari walisema wananifanyia upasuaji wa miguu kwanza na baadaye ndio wataangalia namna ya kunifanyia matibabu ya mgongo ambayo maumivu yake yanatokana na matatizo ya miguu, niliyokuwa nayo," anasema.

Doris anasema, sababu ya kufanyiwa matibabu kwa takribani mwaka mzima, amelazimika kuathirika kimasomo kwamba, anarudia darasa - kidato cha sita mwaka huu kwa matarajio ya kumaliza.

Mwanafunzi huyo anasema, kwa sasa anakabiliwa na changamoto ya usafiri kwenda na kurudi shuleni, kwa sababu anachoka kutokana na hali aliyo nayo.

Matamanio yake binafsi kupatiwa huduma ya hosteli, itakayomrahisishia maisha ya masomo, badala ya kwenda na kurudi shuleni kila siku; Tabata hadi shule ya Jangwani.

**KINAMAMA MOI**

Wanawake watumishi wa MOI, waliguswa na changamoto anayopitia Doris, hivyo katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, mwaka huu, walimpatia kiti cha kutembelea.

Doris anasema, kiti hicho kitamwezesha kuingia na kutoka darasani na kuzunguka maeneo ya shule na maeneo mengine atatumia fimbo aliyopewa kutembelea.

**MAMA YAKE**

Philomena Martin, mama wa Doris, anasema walifika MOI tangu mwaka jana kwa ajili ya matibabu

AFYA

# Aliyetumia vidole, mara ya kwanza atumia nyayo zake

ya shingo na mgongo na walipomfanyia kipimo cha MRI, alibainika kuwa na tatizo la mgongo.

Anasema miguu ya mtoto wake kutokanyaga chini, walihisi ni suala la kawaida, kwa sababu walishazoea kumuona hivyo tangu amezaliwa, lakini alishauriwa kutatua changamoto hiyo.

Philemina anasema baada ya kukubali, walianza vipimo Machi mwaka huu na ikabainika tatizo lipo kwenye miguu, hali inayochangia maumivu.

Anasema walielezwa warudi nyumbani hadi mwezi Mei mwaka jana, walikopangiwa ratiba za kufanyiwa upasuaji na Mei 28, walifanyiwa upasuaji mguu mmoja na alikaa hospitali kwa wiki moja.

Mama huyo anasema, kisha akaruhusiwa kurudi nyumbani, hadi baada ya wiki sita aliporudi tena kufanyiwa upasuaji mguu wa pili.

Philomena anasema Agosti 14 mwaka jana, alifanyiwa upasuaji mguu wa pili na waliruhusiwa kurudi nyumbani na kuanza kufuata ratiba za kliniki kila wiki mara tatu.

Anasema, kwa sasa wamepangiwa kliniki kwa ajili ya mazoezi kwa wiki 40 na kwa namna anavyoona maendeleo ya binti yake. anaamini atapona.



Doris Martin, akiwa katika baiskeli ya wagonjwa aliyonunuliwa na kinamama, watumishi wa Hospitali ya MOI, anakotibiwa. **PICHA ZOTE: MARY GEOFREY.**

### TATIZO LILIVYOANZA

Mama huyo anasimulia, mwanawe alizaliwa bila ya tatizo lolote na alianza kutembea akiwa na miezi tisa, lakini kila alivyokuwa akitembea alilia.

"Nilikuwa sielewi nini maana yake na alipoanza kuongea akawa anasema mama naumia, lakini nikawa sielewi anaumwa vipi.

"Nikaanza kumpeleka hospitali bila ya majibu na madaktari bingwa walivyokuja, nilipeleka wakaniambia tatizo litabainika pindi atakavyoendelea kukua," anasema Philomena.

Anasema madaktari mbalimbali waliofika mkoani Kagera, walimshauri kumsomesha mtoto shule za karibu, ili kumpunguzia uchovu na mtoto wake alipofika darasa la saba, hali ilibadilika akashindwa kutembea bila ya viatu vya mchuchumio.

Philomena anasema, kila mwaka alivyoongezeka, alilazimika kutumia viatu vya mchuchumio mkubwa na alimwongezea soli kadri siku zilivyoongezeka.

Mama huyo anasema ilifika wakati, mtoto huyo alishindwa kubeba begi la madaktari na vitu vizito, hivyo mama huyo alichukua jukumu la kumsaidia.

"Mwanangu aliendelea kwenda shule na viatu vya mchuchumio na walimu na wanafunzi walimwelewa na alipofika kidato cha tano, hali ilizidi kuwa mbaya zaidi. Akaanza kulalamika kuumwa shingo na mgongo," anasimulia mama huyo.

> **Nilikuwa sielewi nini maana yake na alipoanza kuongea akawa anasema mama naumia, lakini nikawa sielewi anaumwa vipi.**

Philomena anasema, binti huyo alipata wakati mgumu wa kufahamu namna ya kumsaidia binti yake, kwa sababu madaktari walimwambia ugonjwa huo hauna dawa.

### ALIVYOHAMISHIWA MOI

Anasema, binti huyo hakupata dawa ya aina yoyote na alipoenda hospitali tena, alihamishiwa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa(MOI), ambako alianza kupatiwa matibabu.

"Namshukuru Rais Dk. John Magufuli, chini ya uongozi wake, aliniwezesha mimi kupatiwa rufani ya kuja MOI mwaka jana na nikaanza matibabu na nilipofika walinilaumu kwanini nilimchelewesha," anaeleza Philomena na kuendelea:

"Kama ningekuwa najua kuna tiba ningewahi kumleta binti yangu, angekuwa ameshapona, naumia kuchelewa kumtibu binti yangu."

### CHANGAMOTO

Anasema, mwanzo alipofika na kuanza matibabu alilazimika kumhamishia katika Shule ya Sekondari Jangwani, ambako anasoma hadi sasa.

Anasema kwa sasa ameanza kwenda shule, lakini anakabiliwa na changamoto ya kuchoka na amekuwa, akimpeleka na kumrudisha nyumbani kila siku.

Mama huyo anaeleza zaidi kuwa, hivi sasa anamfuatilia kupata huduma ya hosteli, lakini anashauriwa kusubiri hadi watakapomaliza wanafunzi wa kidato cha sita.

Akiongea na Nipashe wiki moja iliyopita, ilikuwa wiki ya tatu tangu binti yake alipoanza kusoma katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Jangwani, anakokabiliwa na changamoto ya uchovu na daktari alimzuia kupanda pikipiki, kwa sababu inamuumiza mgongo.

Philomena anasema, kila siku inamgharimu mtoto huyo zaidi ya shilingi 6,000 kwa ajili ya kumpeleka na kumrudisha shuleni.

### WATENDAJI MOI

Katibu wa Umoja wa Wanawake wa Moi, Caroline Soleko, anasema walichanga fedha kupitia umoja wao kwa ajili ya kununua vifaa vya kutoa misaada kwa wagonjwa wao, akiwamo Doris.

Anasema, wameshatoa viti vya kutembelea wagonjwa wawili na msaada kwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi wa Moi na wagonjwa wa saratani, waliopo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Bingwa wa tiba ya mifupa kutoka MOI, Dk. Kenedy Nchimbi, anasema magonjwa ya mifupa ya aina hiyo kwa sehemu kubwa, yanatokana na upungufu katika lishe na anataja vyakula vinavyopaswa kutumiwa zaidi ni maziwa, dagaa, samaki, matunda na mboga za majani, ili kuimarisha mifupa ya binadamu.

### MKURUGENZI MOI

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, anasema wameendelea kuboresha huduma za upasuaji wa nyonga na maeneo magumu, ambayo awali walikuwa hawawezi kufanyiwa upasuaji nchini.

Anasema Februari 14, mwaka huu, kwa mara ya kwanza, MOI, walifanya upasuaji wa maungo ya nyonga na uti wa mgongo kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka nchini India.

Upasuaji huo ulifanywa kwa siku tatu na madaktari bingwa wa MOI na wataalamu kutoka Hospitali ya Zydus ya India na jumla ya wagonjwa sita wenye matatizo magumu ya nyonga na uti wa mgongo walifanyiwa upasuaji.

Anasema Oktoba mwaka jana, waliingia mkataba wa ushirikiano na hospitali hiyo, kwa lengo la kubadilisha uzoefu wa wataalamu, kufanya kambi za upasuaji kwa wagonjwa kama walivyofanya hivi karibuni. Anasema, baadhi wanayoyafanya katika kambi hizo ni kuwaona wagonjwa wa kliniki na kuwafundisha wataalamu wa nchini, kupitia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

Anasema upasuaji huo unahusisha pia, kuunganisha maeneo ambako viungo vimepishana, zikiwamo nyonga ambazo humfanya mtu achechemee.

"Tunatumia vyuma maalum kuviunganisha na mfupa mfupi ili kumfanya ulingane na kurudi katika hali yake ya kawaida kabisa," anasema.

MAZINGIRA

# Baa la njaa kwa maelfu ya wafugaji, minong'ono sasa wanapoteza maisha

## • Mjamzito alalama siku 5 hajala kitu • Mifugo 30,000 yafa...wahamia Uganda • Wanafunzi watoweka ghafla shuleni • Vijiji wameachiwa watoto, wasiojiweza • Serikali: Hakuna vifo, wala njaa kihivyo



Familia ikiwa nje ya nyumba yao wakijitafakari kuhusu njaa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Turkana,** Kenya

WAKATI Wakenya wakiendelea kujadili haja ya serikali kushughulikia ukame, makali ya njaa yanaendelea kushuhudiwa katika Kaunti (jimbo) la Turkana ambayo imekumbwa na ukame.

Kupitia mitandao ya kijamii, wananchi hao wanaitaka serikali kuchukua hatua dhidi ya njaa hiyo inayoendelea kusababisha vifo.

Mjadala unaendelea nchini, huku idadi ya waliokufa kutokana na njaa ikipanda, shule zikilazimika kufungwa, wanafunzi wanawafuata wazazi wao maeneo ya misituni, kutafuta chakula. Kuna wakazi sasa wanahoji katika mitandao ya kijamii, nafasi ya usalama wa chakula kitaifa na namna inavyopatiwa kipaumbele.

Hivi sasa wazee, watoto, wanawake wajawazito na wenye ulemavu, wanaendelea kuumia, kutokana na ukosefu wa chakula na maji.

### MAELFU TAABANI

Inasadikiwa kwamba zaidi ya watu 800,000 wanaendelea kuumia kwa makali ya njaa na kiu, kwa mujibu wa ofisi ya Wizara ya Kudhibiti Majanga na Utumishi wa Umma, katika ya Kaunti ya Turkana.

"Kila kijiji ninachotembelea, nakutana na kinamana na watoto pekee, hali yao ya afya ikiwa imedorora kabisa. Mifupa kwenye miili yao inaonekana ishara kuwa wamestahimili njaa kwa siku kadhaa," anasema mwanahabari Faith Sudi, aliyetembelea eneo la Turkana.

Anasema, hivi sasa hata miti ya miba inayojulikana kustahimili mazingira ya jua na jangwa, imekauka na masomo shuleni yamesimamishwa.

### WANAFUNZI WATOWEKA

Katika Shule ya Msingi ya Lotukumo, iliyoko katika Kaunti (jimbo) ndogo ya Turkana ya Kati, wanafunzi wa darasa la nane (wanaotarajia mtihani) pekee ndio wanaohudhuria masomo, wengine wametoweka.

"Kwa sababu ya ukosefu wa chakula, wanafunzi wengi wanajiunga na wazazi wao kutafuta chakula popote watakapopata. Kwa hiyo, hawawezi kufika shuleni," anasema Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ebong'on Charles.

Darasa la pili ambalo kwa kawaida, huwa na wanafunzi 70, lilikutwa na wanafunzi 11 pekee. Darasa la kwanza halina mwanafunzi kwa muda wa wiki mbili sasa.

Katika kijiji cha Nadoto, nyumba nyingi hazina watu, isipokuwa wajawazito, wakongwe na watoto wadogo.

### MJAMZITO MATATANI

Selina Ebei, ni mama mwenye mimba ya miezi saba, anasema amelazimika kulala siku kadhaa bila chakula, pia ana mtoto mdogo mwenye umri wa miaka miwili anayemtegemea: Anaeleza:

> **Kwa sababu ya ukosefu wa chakula, wanafunzi wengi wanajiunga na wazazi wao kutafuta chakula popote watakapopata. Kwa hiyo, hawawezi kufika shuleni.**



Mama mwenye simanzi ya janga la njaa, akiwa na wanawe.

"Kutokana na hali yangu, siwezi kwenda mwituni kila siku kutafuta matunda ya mkoma kwa sababu ni mbali na jua pia ni kali mno. Wakati mwingine ninakaa siku tano bila kutia chochote mdomoni.

"Mikoma niliyochuma ikiisha, tunakaa njaa tu hadi nitakapojikaza tena kwenda mwituni kuchuma mikoma mingine. Ninambeba huyu mwanangu mgongoni na kutembea mwendo mrefu, kwa sababu hakuna mtu ambaye ninaweza kumwachia amchunge.

"Tunayachemsha na kunywa supu yake na wanaume hawako vijijini, kwa kuwa wameenda na mifugo kwenye milima kuwatafutia chakula," anasema Selina.

### MBUNGE ANG'AKA

Mbunge Mwakilishi wa Wanawake katika Kaunti ya Turkana, Joyce Emanikor, analalamika: "Ni aibu sana watu kufariki kutokana na baa la njaa katika kaunti ambayo inapokea mgao mkubwa wa mapato.

"Serikali ya kaunti iko na ina uwezo mkubwa kuhakikisha wakazi wanapata chakula cha kutosha wakati wa janga kama hili."

Kwa mujibu wa mtazamo wa akiba ya chakula Kenya mwaka huu, baadhi ya maeneo ya mashariki, kaskazini na kaskazini magharibi mwa nchi ambako kuna jamii za wafugaji, huenda zikakabiliwa na uhaba wa chakula.



Bibi Audan Loteng' Takwa (63), akieleza masaibu anayopitia na wanakijiji wenzake ya kuangamia kwa njaa.

Kulingana na ripoti ya Wizara ya Majanga na Huduma kwa Umma ya kaunti ya Turkana, wakazi wengi katika Kaunti ya Turkana hutegemea ufugaji ili kujikimu kimaisha.

Hadi sasa inakadiriwa mifugo 30,000 imeshakufa kwa njaa na mingine zaidi ya 100,000 imehamishiwa nchi jirani ya Uganda.

> **Tumepoteza mifugo mingi kutokana na ukosefu wa usalama, kisha wale mifugo wadogo ambao wamesalia wanakufa kwa ukame.**

"Tumepoteza mifugo mingi kutokana na ukosefu wa usalama, kisha wale mifugo wadogo ambao wamesalia wanakufa kwa ukame. Ni vyema serikali ya kaunti hii irejee bajeti yake, kuhakikisha inazingatia zaidi mahitaji ya wakazi wa eneo hili," anasema Joyce Emanikor.

### SERIKALI YAKANUSHA

Serikali katika taarifa yake, imekanusha madai ya vifo vya watu kunatokana na njaa inayosababishwa na ukame kaskazini magharibi mwa nchi, Waziri wa Tawala za Kaunti, Eugene Wamalwa, akisema havihusiani na ukame.

Mwishoni mwa wiki, gazeti moja liliripoti kuwa watu kadhaa walikufa kutokana na matatizo yanayohusiana na njaa, eneo la Tiaty, Kaunti ya Baringo.

Naibu Rais wa Kenya, William Ruto, anasema Kenya iko katika fursa nzuri kukabiliana na ukame, ikilinganishwa na miaka iliyopita, akiungana na waziri wake kupinga madai ya vifo vya njaa, akisema nchi yake ina chakula cha kutosha na hakuna haja ya kuhofu.

---

# Wazazi wavamia shule kwa vyakula vilivyooza

## • Ni ya kifahari ada mil. 13/-

SHULE moja ya upili ya kifahari nchini China imekosolewa vikali, baada ya kukutwa ikiwa na vyakula vilivyooza ndani ya jiko lake.

Mikate iliyooza, nyama na samaki zilipatikana baada ya wazazi kuvamia shule ya upili ya Chengdu.

Mmoja wa wazazi hao, alieleza namna alivyoshtushwa na harufu kali yenye karaha kutoka kwenye vyakula hivyo.

Uongozi wa shule umeomba msamaha, ikisema kuwa imefedheheka sana na tukio hilo.

Kashfa ya usalama, inaelezwa sio jambo geni nchini China na mara nyingi huzifanya mamlaka husika kukabiliwa na wakati mgumu wa kukabiliana na ghadhabu kutoka kwa umma.

### MKASA ULIVYOKUWA

Kashfa hiyo iliibuka wakati kundi dogo la wazazi likialikwa katika shughuli ya upandaji miti katika shule hiyo kibinafsi mjini Chengdu, katika mkoa wa Sichuan na wazazi hao waligundua kuna mikate iliyooza na vyakula vingine ndani ya chumba kimoja, jirani na jiko la shule.

Haijabainika, ni kwanini waliamua kufika maeneo ya jikoni, wakati shughuli ya upandaji miti haikuwa karibu na sehemu hiyo.

Lakini, mmoja wa wazazi alielezea kuwa mikasa ya wanafunzi kuumwa tumbo na magonjwa mengine, yaliyoripotiwa sana hasa mwishoni wa mwaka jana katika shule.

"Vyakula hivyo vinaonekana kama vilihifadhiwa ndani ya barafu kwa miaka kadhaa," anatamka mmoja wa wazazi aliye na watoto wawili katika shule.

Kwa mujibu wa mzazi huyo, karo ya shule hiyo inagharimu Dola za Marekani 5,800 (Shilingi milioni 13, laki tatu na arobaini) kwa mwaka kiwango ambacho ni karibu mara 20 ya karo inayotozwa na shule za umma nchini China.



Wazazi wakiandamana. Picha ndogo ni; Sehemu ya vyakula vilivyooza. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



"Nasikitika kuwa natumia maelfu ya madola kuwasomesha wanangu katika shule hii, wakati wanalishwa vyakula vilivyooza," anasema mzazi huyo.

### TAARIFA ILIVYOPOKELEWA

Wazazi waliovamia jiko la shule hiyo wakapiga picha vyakula hivyo na kuzisambaza katika mitandao ya kijamii.

Kwa mujibu wa baadhi ya wazazi, shule hiyo ilichukua hatua ya kuondoa vyakula hivyo kwa kutumia magari mawili haraka.

Gari moja lilivamiwa na kuzuiwa na wazazi hao, waliokuwa wakiandamana kuelekea shuleni.

Kanda za video zilizosambazwa katika mitandao ya kijamii siku ya Jumatano wiki iliyopita, ziliwaonyesha mamia ya wazazi walioghadhabika, wakiandamana nje ya lango la shule.

Polisi walionekana wakitumia nguvu za ziada kupita kuwatawanya wazazi hao, huku baadhi yao wakikamatwa na baadaye kuachiwa huru.

Shule hiyo baadaye ilitoa taarifa ya kuomba msamaha na kusema kuwa imesitisha huduma ya watu waliokuwa wakiwaletea vyakula. **BBC**

**• Kwa mujibu wa Mtandao.**

AFYA

AFANDE MPWAGE

# Kilio ukatili wa kijinsia, mtihani unaoanza nyumbani hadi shule

- Wajibu wa mzazi kulea mtoto, si kumtunza
- Kosa; imani yako 'mjomba' alale na mtoto
- Mzazi; unatumiaje faragha, mdomo wako?



Mkaguzi wa Tarafa ya Chang'ombe na Msimamizi wa Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi, kutoka Kituo cha Polisi Chang'ombe, Meshack Mpwage, akizungumza katika warsha hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

UKATILI dhidi ya watoto ni mambo yanayopigwa vita na serikali na wadau wanaotetea haki za watoto, kuhakikisha wanaishi salama.

Ni ukatili ambao Mkaguzi wa Tarafa ya Chang'ombe na Msimamizi wa Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi kutoka Kituo Kikuu cha Polisi Chang'ombe, Meshack Mpwage, anazitaja katika sura nyingi.

Kwa mujibu wa Mpwage, mzazi anapaswa kumlea mtoto na si kutunza, anataja upungufu uliyoko ni katika sura nyingi, akitaja baadhi.

Mpwage anayataja kuwa ni: Mtoto kuhusishwa na mambo makubwa kuliko umri wake; wazazi kulala chumba kimoja na mtoto hata wakaona yasiyomfaa, usimamizi duni wa mavazi ya watoto, wazazi kutokemea mabaya ya watoto wao na mzazi kukataa makosa ya watoto wao, pindi wanapoitwa shuleni kuelezwa.

Katika orodha ya wadau jijini Dar es Salaam, imo asasi isiyo ya kiserikali ya Ekama Development Foundation, inayoendesha mradi wa kuzuia ukatili dhidi ya watoto shuleni na kwenye jamii.

> **"Hatua hiyo inaweza kusababisha ukatili kwao bila ya nyie kujua. Jifunzeni kulea, siyo kutunza. Wanaotunzwa ni mifugo, lakini watoto wanalelewa.**

Kamati zaanzishwa

Katika kutekeleza majukumu yake, ilianzishwa kamati za kuzuia vitendo hivyo, ambazo zinahusisha walimu, wanafunzi na wazazi.

Walimu na wanafunzi wanatoka katika shule za msingi 10 wilayani Temeke, jijini Dar es Salaam.

Hivi karibuni, wadau husika walikutana katika warsha ya utendaji kazi wa kamati hizo na kuelezea changamoto walizo nazo kwa kipindi cha miaka mitatu, tangu ziundwe. Kamati zilitoa taarifa zilizoonyesha kwamba, licha ya kufanya kazi kubwa ya kutoa elimu na kukemea ukatili, bado baadhi ya watu hawabadiliki na wanaendelea na ukatili huo.

**KUTOKA POLISI**

Baada ya taarifa ya kila kikundi, mgeni rasmi katika warsha, Mkaguzi wa Tarafa ya Chang'ombe na Msimamizi wa Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi kutoka Kituo cha Polisi Chang'ombe, Meshack Mpwage, anaeleza kinachochangia kuendelea kuwapo vitendo hivyo.

Mpwage anasema baadhi ya wazazi na walezi wana tabia ya kumaliza kesi za ukatili wa watoto wao kimya kimya, hali inayosababisha ukatili kuendelea kudumu ndani ya jamii.

Anasema mzazi anaweza kupeleka kesi ya vitendo vya ukatili katika kituo cha polisi, ili mashtaka yaandaliwe kwa ajili ya kufikishwa mahakamani, lakini anapoitwa kwa ajili ya kutoa ushahidi hatokei, hali inayosababisha kesi kufutwa.

"Vilevile wazazi msikubali watoto wenu walale chumba kimoja na wageni. Hatua hiyo inaweza kusababisha ukatili kwao bila ya nyie kujua. Jifunzeni kulea, siyo kutunza. Wanaotunzwa ni mifugo, lakini watoto wanalelewa," anasema.

"Inawezekana nyumbani ukawa na vyumba vichache, lakini tafuta njia nyingine ya kumfanya mtoto asilale na mgeni. Huwezi kujua kitakachoendelea chumbani na unaweza kukuta ameharibiwa," anasema.

**WAZAZI LAWAMANI**

Mohamed Panganya, ni mzazi anayerusha lawana kwa wenzake, kwamba wamekuwa chanzo kikubwa cha ukatili dhidi ya watoto, kutokana na tabia zao kama kutoa matusi hadharani.

"Hivi kama mzazi hujiheshimu mtoto wako atajiheshimu? Wazazi wengi hatujiheshimu, tunafanya mambo ya ovyo mbele ya watoto nao wanajifunza kuyafanya wangali wadogo.

Mzazi, Faudhia Nuru, anakemea mavazi mafupi, ambayo baadhi ya wazazi wanawanunulia mabinti zao, ambayo yanawaweka katika mazingira hatarishi kutamaniwa na hata kubakwa.

**WALIMU JE?**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Unubini, Othman Ngakwira, anasema mazingira ya nyumbani kwa watoto, yanachangia ukatili dhidi yao, hasa pale wazazi wanapolala nao chumba kimoja.

Inaelezwa, yawezekana kukawa na baadhi ya mambo ya kiutu uzima, wakidhani wamesinzia, kumbe sivyo. Ni mazingira ambayo mwalimu huyo anasema, yanawafanya watoto kuanza kuwaiga.

Kaimu Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Tandika, Cecilia Ndiskoi, anawaelekezea wazazi lawama ya kuwa wagumu kutoa ushirikiano kwa walimu, pale watoto wanapokutwa na makosa.

Anasema, baadhi ya wanafunzi wanafanya vitendo vya kikatili na wazazi wanapoitwa kuelezwa yaliyotokea, baadhi hawako tayari kutoa ushirikiano, kwa madai kwamba 'watoto wao wanasingiziwa.'

**WAANZILISHI KAMATI**

Mratibu wa Miradi wa Ekama, Hassan Mbilu, anasema asasi hiyo ilifanya utafiti wa ukatili kwa watoto katika shule za msingi 10 mwaka 2015 na kubaini kuwapo ukatili, ndipo wakaamua kuunda kamati zilizoanza kazi ya kuzuia ukatili huo, mwaka 2016.

**MKAKATI SERIKALINI**

Mkurugenzi Msaidizi wa Malezi na Elimu ya Makuzi katika Familia wa Idara ya Watoto, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Grace Muwangwa, alishatamka kwamba Tanzania imeandaa mpangokazi wa kutokomeza ukatili huo kwa kuangalia suala la malezi na ulinzi wa watoto.

Anasema katika utafiti uliofanyika mwaka 2009, ulionyesha asilimia 60 ya wasichana na wavulana wamefanyiwa ukatili wa aina mbalimbali, hali inayoweza kusababisha kuwa na taifa lenye watoto wasio imara.

MAZINGIRA

MKULIMA JOHARI

# Kilimo mseto kimenipatia lishe bora, ardhi rutuba, kipato juu

• Atamba kuiacha njaa, ahamia mlo kamili

Na Beatrice Philemon, aliyekuwa Singida



Wananchi wa kijijini Kibaoni, wakipatiwa mbegu za jamii ya mikunde kutoka shirika la ActionAid Tanzania, kwa ajili ya kilimo mseto. **PICHA: BERATRICE PHILEMON.**

UNAPOTAJA kilimo mseto, msingi wake ni msamiati mmoja, lakini umebeba tafsiri na maana zisizopungua tatu. Kwanza ni uchumi, kurutubisha ardhi, ulinzi wa mazingira na maendeleo binafsi, hususan katika dhana iliyofikia kilele siku chache zilizopita kwamba "wanawake wanaweza, hasa wakiwezeshwa."

Ni tafsiri ambayo uhalisia wake unashuhudiwa katika shughuli za kila siku za mwanamama kijana, Johari Kassim (24), anayepatikana katika Kijiji cha Kibaoni, Kata ya Mudida, Tarafa ya Mtinko, Wilaya ya Singida Vijijini.

Kilimo anachokiendesha, analenga zaidi kuzalisha mazao mengi katika eneo moja na kwa wakati mmoja, huku akihakikisha mazingira ya ardhi yake yanabaki vilevile.

Hilo linafanyika, akijianika mbele ya jamii kwamba yeye ni mwanamke anayeweza na amejitanua kufikia kiwango cha mwalimu wa kilimo mseto kwa wanakijiji wenzake

Kipi anachokifanya? Jibu liko bayana, kwamba ni kilimo ambacho kitaalamu kinatafsiriwa ni: Mchanganyiko wa mazao mengi au mbalimbali kwenye shamba au eneo moja mtu anakolima.

Kilimo mseto kinafanyika katika jamii ya mikunde na faida yake inarutubisha ardhi na mavuno yanakuwa mengi au mbalimbali, kwenye shamba au eneo moja

"Hapo awali, sikujua nini maana ya kilimo mseto. Sikujua nini maana ya kumpa mtoto vyakula vyenye virutubisho, kwa sababu mtoto akila vyakula vyenye virutubisho, anakuwa kiafya na kiakili, mchangamfu, mcheshi na anakuwa mkakamavu," anasema.

Pia, anataja kuwa imemwongezea kipato, uzalishaji wa tija na matumizi sahihi ya mazao ya jamii ya mikunde, anasema inachangia kuwaongezea watoto vitamin, pia watu wazima.

### SAFARI YA JOHARI

Johari anasema, baada ya kujiunga na mradi wa Kilimo Mseto na Lishe Singida (SNAP), unaofadhiliwa na asasi ya McKnight Foundation kutoka USA, maisha yake yalianza kubadilika, baada tu ya kupata mafunzo ya uendeshaji wake.

"Kwanza kabisa nilianza kupata chakula cha kutosha kutokana na elimu niliyoipata ya kilimo mseto, kwa sababu kwenye kilimo mseto, tulifundishwa namna ya kuboresha ardhi kwa kuandaa masalia ya mimea shambani.

"Pia, namna ya kupanda mazao yanayotambaa kwa ajili ya kutunza unyevu, ili mimea yetu isiharibiwe na ukame, mazao kama vile maboga, mikunde, maharage yaani jamii ya mikunde kwa ujumla kwa sababu mimea hii inaongeza lishe katika udongo," anaeleza.

> **Tofauti iliyopo kati ya nyama nyekundu na nyeupe inaonekana zaidi katika umeng'enywaji tumboni. Nyama, nyeupe inameng'enywa kirahisi, ikilinganishwa na nyekundu.**

Pia, anakiri kuwa watoto wake hivi sasa wanasoma vizuri, maisha yake yamebadilika sana, kipato kimeongezeka na kumsaidia kuongeza ekari nyingine kwa ajili ya kilimo hicho mseto.

"Tunashukuru Shirika la ActionAid Tanzania kutuletea mradi huu katika kijiji chetu, kwa sababu kupitia mradi hivi sasa hali ya kilimo katika kijiji chetu imeanza kuboreka," Johari anasema.

Anaendelea: "Wakulima wanajua matumizi sahihi ya mazao ya jamii ya mikunde kama inaongeza Vitamin A kwa watoto na watu wazima."

### WAKULIMA WABADILIKA

Mama huyo anasema, pia amewahamasisha wakulima wa jinsia zote kujikita katika kilimo mseto, kwa sababu kinazalisha mazao mengi ya kutosha katika eneo au shamba moja, pia kinarutubisha udongo.

Ni namna ambayo Johari anafafanua kuwa manufaa yake ni kwamba, katika mjumuiko huo una manufaa ya mtu anapokosa zao moja, anapata lingine katika eneo moja la kilimo.

Vilevile, wananchi wameshaanza kula vyakula vyenye virutubisho vya kutosha na afya za watoto na watu wazima zimeboreka kwa kula vyakula mchanganyiko.

Johari anasema, katika miaka iliyopita kabla ya kuanzishwa mradi, wananchi waliegemea kula vyakula vya wanga zaidi, akitaja mlo wa ugali na mlenda, anavyovieleza si lishe inayojitosheleza kwa watoto na watu wazima.

Mradi wa SNAP ulianzisha elimu hiyo kwa wananchi, lengo ni kuboresha udongo na afya za umma, kwa kutumia mimea jamii ya mikunde, kuongeza uzalishaji, kuboresha udongo, ongezeko la kuwasaidia kulima kilimo kwa njia ya kisasa.

### MAFUNZO WALIOPATA

"Wakati wa mafunzo tulifundishwa kulima mazao mchanganyiko, pia namna ya kuboresha ardhi kwa kuacha masalia ya mimea shambani na kutochanganyisha shambani," anasema.

Vilevile, walifundishwa namna ya kupanda mazao yanayotambaa kwa ajili ya kutunza unyevu na mimea isiharibike na ukame, mfano hai ukiwa maboga, kunde na maharage, kwa sababu inaiongezea lishe udongo.

Eneo lingine la funzo kwa mujibu wa Johari, ni kutengeneza vyakula mbalimbali vyenye virutubisho kwa lishe ya watoto na familia, hapo ikitajwa mifano ya maboga, viazi lishe na mengine jamii ya kunde.

### UWAJIBIKAJI KIJINSIA

Ni programu inayotajwa na Johari kwamba, pia walipata darasa la mgawanyo wa majukumu katika familia na wakafahamu namna gani familia inaweza kushirikiana katika mambo mbalimbali, ikiwamo majukumu makuu ya baba na mama, katika mambo ya kifamilia.

"Tulijifunza baba kumsaidia mama kazi za nyumbani, kipindi mama ananyonyesha au mjamzito. Pia, tulijifunza unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi na upendeleo," anaongeza.

Katika utengenezaji wa vyakula vya lishe, kama vile zao la kunde, walifundishwa kutengeneza bagia, kupika kunde, namna kunde inaweza kuchemshwa na kutumiwa kama mboga.

Kwa upande wa mbaazi, unaweza kutengeneza uji, kutengeneza biskuti, kuzikaanga na kula kama karanga au kutumia kama kande, kwa mtu anayependa kula mbaazi, mbaazi ina vitamin A nyingi sana walituambia walimu.

"Wameamua kutufundisha kuwapa watoto vyakula vya jamii ya mikunde, kwa sababu watoto wengi katika nchi mbalimbali za Afrika, wanatumia mboga za asili ambazo hazina virutubisho vyovyote kama vile mlenda wa kusaga," anasema.

### UPATIKANAJI MBEGU

Ni mradi ulioendana na asasi ya ActionAid Tanzania, kuwapatia mbegu za jamii ya mikunde kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Ilonga na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Mikocheni (MARI), ili

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Dk. Ndugulile: Upandikizaji figo nchini umenusuru Sh. bilioni 4.2

• Huduma zapatikana Dar na Dodoma



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Faustine Ndugulile (kushoto), akimjulia hali mgonjwa wa figo, aliyelazwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

MATIBABU ya ugonjwa wa figo, awali yaliigharimu serikali kutumia mamilioni ya fedha kwa ajili ya kuwapeleka Watanzania nje ya nchi kupatiwa matibabu hayo.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeamua kujikita katika upatikanaji wataalamu wanaopandikiza figo na kufanikisha huduma hiyo itolewe nchini, ikihama kutoka utaratibu wa awali, serikali ikitumia pesa nyingi kuwapeleka nje ya nchi Watanzania kutibiwa figo.

> **Hivi ninavyoongea, tayari mgonjwa mmoja amekwishapandikizwa figo na ameshatoka salama.**

Hivi karibuni Hospitali ya Benjamin Mkapa ya jijini Dodoma, imefanikiwa kupandikiza figo jumla ya wagonjwa saba, tangu ilipoanza kufanya huduma hiyo, kwa kushirikiana na madaktari kutoka Shirika la Afya la Tokushukai la nchini Japan.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika ziara yake ya kukagua hali ya utoaji huduma za kibingwa za magonjwa ya figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, Dk. Ndugulile, anasema kuwa idadi ya wagonjwa waliokwishapandikizwa figo nchini imefikia 43.

Anasema, watu 38 walipatiwa huduma hiyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na wagonjwa watano, katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

"Hivi ninavyoongea, tayari mgonjwa mmoja amekwishapandikizwa figo na ameshatoka salama, yupo anaendelea kuangaliwa.

"Lakini, wana mpango wa kuwafanyia wengine wawili. Tutapokuwa tumekamilisha hili, tutakuwa na wagonjwa saba ambao wamefanyiwa upandikizaji," anaeleza.

Anasema kwa sasa, serikali inalenga kuhakikisha inawajengea uwezo wataalamu wa ndani kufanya upasuaji wa kibingwa, ili wawahudumie Watanzania nyumbani, bila ya msaada wa wataalamu wa kigeni.

"Kusudio ni kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo wa ndani wa kuweza kufanya upasuaji huu," anasema Dk. Ndugulile, anayeongeza kuwa serikali imeshaokoa zaidi ya shilingi bilioni 4.2 ambayo ingetumika kutibu wagonjwa kati ya 80 hadi 100, ambao wangepelekwa nje ya nchi kutibiwa.

Katika hilo, Dk. Ndugulile, anaelekeza shukurani kwa wataalamu kutoka Shirika la Tokushukai la nchini Japan, waliojitolea kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani, hali inayosaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa fedha ambazo zingeenda kwa wanaoenda kutibiwa nje.

"Kwa niaba ya serikali ya Tanzania, nimepita kuwashukuru na kuwapongeza, kwa sababu badala ya kutusaidia sisi samaki, wenzetu wa Japan wameamua kutupatia sisi mishipi na kutufundisha jinsi ya kuvua. Naamini ujuzi huu utatusaidia sana," anatamka naibu waziri, alipokuwa jijini Dodoma.

Bakari Juma, ni mkazi wa Dar es Salaam, anayesema kuwapo huduma hiyo, kunampa faraja ya matarajio ya kuipunguzia serikali mzigo wa kutumia fedha nyingi kuwapeleka raia wake nje ya nchi kufuata huduma hizo.

Anasema, elimu ya ulaji vyakula, inapaswa iendelee kutolewa ili iwafikiwe Watanzania wengi kwa manufaa ya wabaki salama kiafya.

Kwa mujibu wa Bakari, ulaji usiofaa unachangia kuleta magonjwa yasiyo ya kuambukiza, yanayohatarisha afya na hata kusababishia kupita magonjwa ya figo.

# Kilimo mseto kimenipatia lishe bora, ardhi rutuba, kipato

**INATOKA UK.19**

kupanda katika maeneo yetu ya kilimo.

Baada ya kutolewe mafunzo hayo, ndipo zilipochukuliwa mbegu za kilo mbili kila moja kwa mazao ya karanga, kunde, maharage na zikapandwa kwenye shamba la ekari mbili.

"Niliandaa shamba vizuri kwa kusafisha, nikalibomoa vizuri na nilianza kulima kilimo mseto, hatua moja hadi nyingine kwa kufuata urefu sentimeta 30, na upande mwingine sentimeta 90," anasema Johari.

Anataja mavuno yake katika msimu wa kilimo mwaka 2016, aliyotumia kwa chakula cha familia ni: Mbaazi debe tatu; kunde debe mbili; karanga debe sita; na maharage ya njano gunia moja.

Johari anaema, katika msimu wa kilimo 2017/2018, aliboresha kilimo chake kwa kupanda mbegu za mahindi, kunde na karanga, ambazo katika kila ekari moja alifanikiwa kupata gunia 17 za mahindi; debe tano za kunde; na karanga gunia moja.

Analeza kuwa, mavuno ya kunde aliwauzia wananchi kwa ajili ya mbegu, kwa sababu wakulima wengi walihitaji mbegu na alipata shilingi 40,000, alizotumia kununua vyakula vya nyongeza, ambayo hakuwa navyo.

Miongoni mwa mazao hayo ya lishe anayataja kuwa ni mchele, mahindi na karanga, aliyotumia kwa mlo. Kupitia mradi wa SNAP, jumla ya vijiji 20 vimeshanufaika kuboresha afya za watoto wao na ardhi ya kilimo nayo imeboreka, huku Johari akijivuna kwamba, maisha yake binafsi yameboreka.

**MATARAJIO YAKE**

Johari anasema, kwa sasa matarajio yake ni kuzalisha mazao ya jamii ya mikunde kwa wingi, kwa sababu ndiyo ambayo watu wengi hawayajatilia mkazo katika uboreshaji wa afya za watoto wao na watu wengine.

"Nataka kuzalisha mbegu za jamii ya mikunde kwa ajili ya kuuza kwa wakulima, ila nataka kupata ujuzi zaidi jinsi ya kuzalisha mbegu na mbolea," anasema.

Ombi lake ni kwa ama Wizara ya Kilimo au ActionAid Tanzania, kuwasaidia kupata wataalamu wa kuwafundisha wao wakulima, namna ya kuzalisha mbegu na mbolea.

Anasema, binafsi ataendelea kuihamasisha jamii katika wilayani Singida, ijikite kwenye kilimo mseto, kwa sababu ni cha uhakika katika upata mazao kwa wingi na kuinua uchumi wa mwananchi, mmoja mmoja.

"Hivi sasa hivi nina mashamba ya kilimo biashara zaidi ya ekari 10 na lipo mbugani. Shamba hili nilinunua mwaka 2017, baada ya kupata kipato kizuri na kuzalisha kwa tija kupitia mradi wa 'Singida Nutrition and Agro-ecology Project (SNAP)' unaoendeshwa na ActionAid Tanzania," anasema.

**MJUE JOHARI**

Johari Kassim ni mkulima na mama wa watoto wawili, anayeishi katika Kijiji cha Kibaoni, Kata ya Mudida, Tarafa ya Mtinko Wilaya ya Singida Vijijini.

Johari alimaliza elimu ya sekondari mwaka 2012 na baada ya hapo, alipumzika nyumbani mwaka mmoja ndipo alipofunga ndoa.

"Nilitamani sana kwenda kusoma, lakini wazazi wangu hawakuwa na uwezo wa kunisomesha. Wazazi wangu ni wakulima na wafugaji wenye kipato cha chini," anaeleza.

Anasema baada ya kuolewa maisha yake yalikuwa magumu kidogo, kwa sababu hali ya maisha haikuwa rafiki, hasa kwenye suala la chakula cha kutosha kumfikisha kipindi cha mavuno ya msimu uliofuata.

"Sijawahi kulala njaa, ila nilikuwa napata chakula kwa shida, kwa mfano ilifikia hatua nilikwenda kutafuta kazi ya kibarua, ili nifanye kazi na kupata hela ya kununua chakula kwa ajili ya familia yangu," anasema.

Johari anasimulia, kwamba alipojitolea kulima katika shamba la mtu, alilipwa shilingi 30,000 kwa ekari na alilima kwa muda wa siku nne.



## HABARI MBEYA

# CCM wavuna wapiga debe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAPIGA debe wa mabasi ya daladala jijini hapo wameshauriwa kuanzisha Chama cha Akiba na Mikopo (Saccos) ili kujiwekea akiba kwa ajili ya maendeleo na kuepuka kuwa wategemezi.

Hayo yalisemwa jana na Mdau wa Maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, wakati viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini walipokuwa wanawakabidhi vijana hao kadi za uanachama katika kituo cha daladala cha Kabwe.

Mwaselela ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Uchumi na Fedha ya CCM Mkoa, aliwapatia vijana hao shilingi milioni moja kwa ajili ya kufanyia taratibu za kuanzisha saccos hiyo ikiwa ni pamoja na kuisajili na kuhamasisha wapiga debe kujiunga.

Aidha, aliahidi kuwachangia shilingi milioni nne kama mtaji endapo watafanikiwa kuisajili na kwamba atawasaidia kukamilisha baadhi ya taratibu kama alivyowasaidia waendesha pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) ambao tayari wameshaanzisha saccos.

Alisema vyama vya aina hiyo huwa vinasaidia kukabiliana na changamoto ndogo ndogo za maisha ikiwamo kusaidiana endapo mmoja wa wanachama anapokuwa amepata matatizo.

"Mimi ni msela mwenzenu, mtoto wa mama ntilie kwa hiyo nitakuwa tayari kuwasaidia ili kuhakikisha chama chenu kinakuwa na nguvu na mnanufaika, kwa sasa nawashauri muanze taratibu za kusajili na mkishamaliza mniambie ili niwaletee milioni nne za mtaji," alisema Mwaselela.

Aliwataka maofisa hao kufanya kazi zao kwa nidhamu ikiwamo kuepuka vurugu ambazo huwa zinawafanya waingie kwenye migogoro na serikali pamoja na wasafiri ambao ndio wateja wao wanaowafanya wapate fedha.

Hata hivyo Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya, Afrey Msomba, alisema kitendo cha vijana hao kuanzisha saccos hiyo kitakuwa ni njia mojawapo ya kujikwamua kiuchumi na kutokuingia kwenye makundi maovu.

Alisema kuna baadhi ya vijana ambao wamekosa mitaji, lakini kupitia saccos hiyo wanaweza kujikopesha wao wenyewe na kuendelea kuanzisha biashara zitakazo waingizia kipato huku wakiendelea na shughuli yao ya kupiga debe.

# Taasisi yakutanisha wakulima kuwapa mafunzo ya kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Uyole ya jijini Mbeya imeanza kuimarisha kilimo kwa kuwakutanisha wakulima kutoka maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kuwapa mbinu za kilimo bora pamoja na teknolojia za kisasa za uzalishaji.

Wakulima hao wanafundishwa zaidi uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara yakiwamo mahindi, maharage, viazi mviringo, vitamu na lishe, ngano pamoja na maparachichi, huku lengo likitajwa kuwa ni kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Tari- Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema wameamua kuanza kupeleka teknolojia hizo kwa wakulima ili kuwezesha azima ya serikali ya kufikia uchumi wa kati inafikiwa.

Alisema awali walikuwa wanatoa elimu na teknolojia kwa wakulima baada ya mavuno, lakini wakabaini kuwa mfumo huo hauna tija kutokana na teknolojia hizo kutowafikia wakulima kwa ufasaha na hivyo wakaona ni vema waanze kuwafuata mashambani.

Dk. Bucheyeki alisema baada ya kufanya utafiti walibaini kuwa wakulima wanashindwa kuzichukua teknolojia wanazofundishwa kwa sababu hazielezewi thamani yake kwa mfumo wa fedha, hivyo wakaona ni bora wawaeleze wakulima kuwa akilima na kupanda kwa kutumia teknolojia hizo watapata fedha kiasi fulani.

"Sasa tumeanza na wakulima pamoja na vikundi vyao na tumeanza kuwaeleza kuwa ukilima mahindi, ngano, maharage, viazi na soya na kwa kutumia mbegu zinazozalishwa na watafiti watapata kiasi fulani cha fedha kwa eneo ili wahamasike zaidi," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisisitiza kuwa kituo hicho kinazalisha mbegu kulingana na hali ya hewa na mazingira ya eneo ambalo mbegu hizo zinapandwa ili kuwarahisishia wakulima.

Ofisa Kilimo Mtafiti wa Tari-Uyole anayeshughulikia mahindi, Bonface Minja, alisema kwa sasa mafunzo ya kilimo ni muhimu kwa wakulima kutokana na mahitaji ya serikali ya kufikia uchumi wa viwanda ambao unahitaji malighafi za kutosha na zenye ubora.

Alisema teknolojia wanazofundishwa wakulima ni kwa ajili ya kuongeza tija kwenye mazao wanayozalisha ili chakula kipatikane kwa wingi na malighafi kwa ajili ya viwanda zipatikane.

Minja alisema wakulima wengi wanakosea kwenye uzalishaji kwa kutumia teknolojia zilizopitwa na wakati hali inayowafanya wasipate tija inayotarajiwa na hivyo akawashauri wazingatie teknolojia mpya wanazofundishwa.

"Tunawafundisha waachane na kilimo cha mazoea, matumizi sahihi ya mbolea, mbegu za kisasa, matumizi sahihi ya viuatilifu ili mazao yao yasishambuliwe na wadudu pamoja na upandaji wa kufuata vipimo sahihi," alisema Minja.

Alisisitiza kuwa kila zao lina aina yake ya udongo, hivyo akawataka wakulima kuwa na utaratibu wa kupima ardhi ya mashamba yao kujua aina ya virutubisho vilivyomo. Baadhi ya wakulima waliohudhuria mafunzo hayo kutoka mikoa mbalimbali walisema watatenda kuzitumia mbinu walizofundishwa, ili kuongeza tija kwenye kilimo chao kwa madai kuwa kilimo cha mazoea kimekuwa kikiwaumiza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Charles Itembe, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuwahakikishia wateja wake ubora wa huduma baada ya kuinunua Benki M. Wengine kutoka kulia ni Mkurugenzi wa Mikopo, Esther Mang'enya na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara, Rhino Nyansaho. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Mawasiliano yakatika baada ya daraja kuvunjika

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MAWASILIANO kati ya Mkoa wa Mbeya na Tabora kupitia Chunya, yalikatika kwa muda baada ya daraja la Mto Lupa linalounganisha Chunya Mjini na Mji Mdogo wa Makongolosi kuvunjika na hivyo kusababisha magari yashindwe kupita.

Tatizo hilo lilitokea juzi, ambapo daraja hilo lilivunjika baada ya Mkandarasi wa Kampuni ya China Railway 15 Bureau Group Corporation Ltd anayejenga barabara ya Chunya- Makongolosi yenye urefu wa kilomita 39 kwa kiwango cha lami kupitisha gari iliyokuwa imebeba mzigo mzito kuliko uwezo wa daraja.

Kufuatia tatizo hilo wataalamu kutoka Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Meneja, Mhandisi Eliazary Rwekiza, walifika katika eneo hilo pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Chunya kwa ajili ya kunusuru hali hiyo.

Mhandisi Rwekiza, alimpa siku tatu mkandarasi anayejenga barabara hiyo pamoja na mkandarasi mshauri kuhakikisha analirejesha daraja hilo katika hali ya kawaida ili liendelee kupitika na wananchi waendelee kufanya kazi zao kama kawaida.

Alisema wao kama wasimamizi wa barabara baada ya kupata taarifa waliamua kwenda mara moja katika eneo hilo ambalo lipo umbali wa kilomita 83.5 kutoka Mbeya Mjini kwa ajili ya kujionea hali ilivyo na wakaamua itengenezwe njia mbadala ya kupita chini ya maji.


"Tumetengeneza hapa chini ili mawasiliano yafunguke, kesho (jana) tutaendelea kurekebisha hili daraja ili lirudi katika hali yake na niseme wazi kuwa hili ni jukumu la mkandarasi kutokana na mkataba wake na jukumu lake ni kuhakikisha anatekeleza maelekezo," alisema Mhandisi Rwekiza.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Chunya ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi, alisema hakuna madhara yoyote ya kibinadamu yaliyotokea kutokana na kuvunjika kwa daraja hilo.

Mahundi aliwataka watumiaji wa barabara hiyo kuwa makini kwa kufuata alama zilizowekwa na mkandarasi ili kuepuka ajali ambazo hazina ulazima.

Alisema chini ya daraja hilo maji yanayopita ni mengi hasa mvua ikinyesha, hivyo akawataka watumiaji kuwa makini ili kuepuka madhara wakati daraja likiendelea kurekebishwa na mkandarasi ambaye tayari alikuwa ameshapewa maelekezo.

Alisema baada ya kutengeneza njia mbadala ya kupita kwenye maji, magari yote yaliyokuwa yamekwama katika eneo hilo yalipita na kuendelea na safari, lakini akatahadharisha watumiaji kuwa makini wanapopita.





# Waganga wa mikoa wepewa mtihani fedha za serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka waganga wakuu wa mikoa kuhakikisha wanasimamia fedha zitakazotolewa kwa ajili ya uendeshaji na utekelezaji wa mradi wa huduma jumuishi za afya ya uzazi.

Agizo hilo lilitolewa jijini hapo jana na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Sudi, wakati akizindua mradi huo.

Alisema mradi huo utatekelezwa kwa miaka 10 na utaanzia 2019-2022 na kuwataka kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema lengo ni kuona kila mkoa unafanikisha zoezi hilo kutokana na kwamba una madhumuni ya kuzuia na kujenga afya kwa jamii.

"Hapa niyapongeza mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo ni wadau katika mradi huu wakiwamo UMATI, DMI, OPTIONS na Maria Stopes Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele kulinda na kuendeleza afya," alisema.

Aliitaja mikoa ambayo inatarajiwa kufikiwa kuwa ni Katavi, Mara, Iringa, Dodoma, Tabora, Mbeya, Songwe, Singida, Kilimanjaro na Dar es Salaam.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa mikoa iliyochaguliwa ina uhitaji mkubwa wa huduma hiyo ndiyo maana imepewa kipaumbele.

Alisema lengo ni kuona wanafika sehemu husika ambazo zimetajwa na serikali inachokitaka ni uwazi na kuagiza kitengo cha afya Tamisemi kishirikiane na kitengo cha afya ya uzazi na mtoto waweke mipango hiyo vizuri ili mradi huo ufanikiwe.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Waganga Wakuu hao, Dk. Charles Kiologwe, alisema watahakikisha wanasimamia hatua zote stahiki kuhakikisha wanafanikisha mradi huo.

# Changamoto usajili vizazi, vifo zawekwa hadharani

**Na Elisante John,** SINGIDA

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini nchini (RITA), umesema changamoto zinazowakabili wananchi wa Mkoa wa Singida kwenye usajili wa vizazi na vifo zinaweza kutatuliwa endapo watapata elimu ya umuhimu wa matumizi ya nyaraka hizo.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Habari wa RITA, Jafari Malema, wakati wa mafunzo ya waandishi wa habari wa mkoa huo, jijini hapo.

Alisema wakala huo kwa sasa unaendesha zoezi la utoaji vyeti kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano kwa mikoa 13 nchini.

"Huduma za usajili wa watoto hao, hivi sasa serikali imezisogeza karibu na maeneo ya wananchi, ikiwamo ofisi za kata na vituo vya kutolea huduma za afya, tena bila ya malipo yoyote... waandishi mna jukumu kubwa la kuwahabarisha ili washiriki kikamilifu," alisema.

Malema alifafanua kuwa mafunzo kwa waandishi hao hayalengi kuripoti kampeni hizo pekee, bali wanapaswa kufahamu kwa undani taratibu zinazohitajika katika kufanikisha zoezi hilo.

Alisema kuwa iwapo waandishi wataelewa kwa kina faida za jamii kuwa na cheti cha kuzaliwa, watakuwa wameshiriki kwa ufanisi kuandika taarifa sahihi, ambazo hazitapotosha umma, hivyo kufanikisha kampeni hiyo muhimu kitaifa.

Alizitaja baadhi ya faida za kuwa na cheti hicho kuwa ni utambulisho wa awali kisheria utakaomwezesha mtoto kupata haki ikiwamo kuandikishwa shule ya msingi na sekondari, kupata mikopo ya elimu ya juu na kupata ajira kwenye taasisi za serikali.

Aidha, Malema alisema kuwa ili mtoto aweze kusajiliwa, ni lazima mzazi afike kwenye kituo cha usajili, akiwa na kiambatanisho cha barua ya mtendaji wa kata, nakala ya kadi ya kliniki au tangazo la kizazi.

Kwa mujibu wa takwimu ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, ni asilimia 9.3 tu ya watoto wa mkoa wa Singida na asilimia 7.7 kwa Dodoma, walisajili na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.




Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi (kushoto), akiwatangazia waandishi wa habari (hawapo pichani) njia za mabasi zitakazotumika kutoka mjini hadi mji wa kiserikali ulioko Ihumwa jijini Dodoma. Kulia ni Ofisa Mfawidhi Mkoa wa Dodoma, Mohamed Zander. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waagizaji, wauzaji kemikali wapewa angalizo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAAGIZAJI na wauzaji wa kemikali wametakiwa kuzingatia sheria wanapoingiza kemikali hizo nchini ili kuepusha madhara.Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja wa Kanda ya Kati Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Musa Kuzumila, katika semina ya wadau iliyofanyika jana jijini hapa.

Kuzumila aliwataka waagizaji na wauzaji wa kemikali kuzingatia sheria za kuagiza na uhifadhi wa kemikali ili kuepusha madhara kwa jamii.

"Hizi kemikali ni sumu mnapoagiza au kuuza hakikisheni mnazingatia sheria ya uhifadhi wa kemikali hizo ili kuepusha madhara ya kiafya kwa jamii yanapoingia kutumika," alisema.

Meneja huyo alisema semina hiyo inajumuisha mikoa mitano ya kanda ya kati ambayo ni Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora na Iringa.


Alisema lengo la semina hiyo ni kutoa mafunzo na kuwakumbusha waagizaji na wasimamizi wa kemikali za viwandani na wajasiriamali wanaozalisha bidhaa zao kwa kutumia kemikali kuhakikisha wanazitunza kwa uangalifu pamoja na watu wa migodini.

Aidha, alisema katika semina hiyo ofisi hiyo imewashirikisha walimu wa masomo ya kemia kwa shule za sekondari kwa kuwa wanafunzi wanatumia kemikali katika masomo yao.

Kwa upande wake, Mratibu wa Kituo cha Kudhibiti Matukio ya Sumu kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Josephine Kalima, alisema kwa muda mrefu walikuwa Idara chini ya Wizara ya Afya, hadi tarehe 26 Machi 1999, ilipobadilishwa na kuwa Wakala wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzisha Wakala za Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997.

Aliongeza kuwa mnamo Aprili 5, 2017, maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilitangazwa kuwa mamlaka chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Na.8 ya Mwaka 2016.

Alisema dhima ya mamlaka hiyo ni kutoa huduma bora za kimaabara kwa gharama nafuu, kutoa ushauri na kufanya utafiti wa kisayansi na kutoa huduma kwa serikali, taasisi na watu binafsi kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira.





Meneja wa Zantel Kanda ya Pemba, Yakub Fadhil (kulia), akimkabidhi mshindi wa kwanza wa mwezi wa promosheni ya Tumia EzyPesa Ushinde, Abdallah Salum (kushoto), kitita cha mamilioni mwishoni mwa wiki mjini ChakeChake. Kupitia promosheni hiyo ya miezi 3 watumiaji wa huduma za kifedha ya EzyPesa wataweza kujishindia fedha taslimu na simu za mkononi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajivunia uhusiano na Cuba utoaji huduma za afya

**Na Rahma Seleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya Zanzibar, Asha Ali Abdulla, amesema Cuba ina historia ndefu katika sekta ya afya ambayo inaweza kuendelea kutoa funzo kwa Zanzibar iliyojipanga kuimarisha miundombinu itakayowezesha kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wake.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na wakurugenzi wa wizara yake, pamoja na uongozi wa taasisi ya kitaifa ya utafiti na matibabu ya maradhi ya saratani na mionzi ya nchini Cuba kwenye makao makuu ya taasisi hiyo, mjini Havana Cuba, akiwa katika ziara ya siku nne ya kujifunza mbinu na masuala mbalimbali ya afya.

Alisema Zanzibar tayari imeanzisha kitengo kidogo cha matibabu ya saratani katika kipindi cha hivi karibuni ambacho kitahitaji kupata msukumo wa kitaaluma kupitia wataalamu waliobobea wa fani hiyo.

Alisema kitengo cha tiba ya maradhi ya kansa kwa Zanzibar bado kipya ambacho wataalamu wa Cuba wanaweza kusaidia mbinu na taaluma katika kuona mpango huo unafanikiwa kwa faida ya ustawi wa wananchi wote.Aliongeza kuwa juhudi zimechukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya katika kukiimarisha kitengo hicho kwa kuwapatia mafunzo ya juu madaktari watatu wa kutibu maradhi ya saratani ili ifikie hatua ya kuwa na wataalamu wake katika azima ya kuwaondoleo usumbufu wananchi wake kufuata huduma hiyo nje ya Zanzibar.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Utafiti Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Mayasa Salum, aliushauri uongozi wa taasisi hiyo, kujenga ushirikiano na Zanzibar katika masuala ya utafiti, ufundishaji wa madaktari pamoja na wauguzi ambao wako katika kitengo cha saratani.

Dk. Mayasa alisema ushirikiano wa pamoja baina ya taasisi ya utafiti wa afya ya Zanzibar na ile ya Cuba unapaswa kuelekezwa pia katika dawa asili za mitishamba ambazo zinaweza kusaidia tiba ya saratani. Mapema Mratibu Mtaalamu Mkuu wa Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti na Utibabu wa Maradhi ya Saratani na Mionzi nchini Cuba, Profesa Lorenzo Anasagasti, alisema taasisi hiyo imeasisiwa mnamo mwaka 1945, ikilenga kuimarisha afya za wananchi wake. Profesa Lorenzo alisema hatua mbalimbali za utafiti zilianza kuchukuliwa baada ya kutokea kesi ya kwanza ya maradhi ya saratani mnamo mwaka 1637 katika kukabiliana na changamoto zinazosababisha maradhi hayo.

Alisema madaktari wa Cuba wameanza safari ya kujiingiza katika utafiti wa kina kufuatia kuanzishwa kwa chuo cha sayansi chini ya madaktari mabingwa kutoka Uingereza, Ujerumani pamoja na Ufaransa kwa kutumia vifaa vya teknolojia ya kisasa.

Alieleza kwamba utaalamu wa kutumia mionzi kwa kutibu maradhi ya kansa uliongezeka zaidi mnamo mwaka 2014 na kusaidia kutibu wagonjwa kutoka nchi 14 duniani yakiwamo mataifa ya Bara la Afrika.

# Rais Shein aimwagia sifa UN

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameupongeza Umoja wa Mataifa (UN) kupitia programu yake ya kujitolea ya umoja huo (UNV) kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika shughuli za maendeleo.

Dk. Shein aliyasema hayo Ikulu mjini Zanzibar, wakati alipofanya mazungumzo na Mratibu Mkuu wa Programu ya Kujitolea ya Umoja wa Mataifa (UNV), Oliver Adam, aliyefika Zanzibar kwa lengo la kuimarisha ushirikiano baina ya pande mbili hizo.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Shein alimweleza mratibu huyo kuwa (UNV) ni programu muhimu iliyo chini ya Umoja wa Mataifa ambayo ina umuhimu mkubwa katika kuendeleza shughuli mbalimbali za maendeleo Zanzibar.

Alieleza kuwa programu hiyo imeanza miaka mingi na kuweza kusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza na kuunga mkono juhudi za serikali katika shughuli za maendeleo ikiwamo sekta ya afya, kilimo na sekta nyenginezo. Aidha, Dk. Shein alimweleza mkuu huyo kuwa tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha kituo cha ujasiriamali ambacho kinatoa mafunzo kwa vijana ya kazi za aina mbalimbali za ujasiriamali, ambapo kuna haja ya kukiongezea uwezo pamoja na kuwapatia mtaji vijana hao ili wanufaike na elimu wanayoipata.

Alisisitiza kwamba kuna haja ya kuweka mikakati maalum ya kuwajengea uwezo vijana wote wa Unguja na Pemba ili waweze kujiajiri wenyewe kwa kuwapa mikopo midogo midogo itakayowasaidia kujiendeleza na hatimaye kujiajiri.

Alisema programu hiyo ya (UNV) kuunga mkono katika kuongeza nguvu kwa kupata walimu wa masomo ya sayansi kwa skuli za sekondari za Zanzibar ambao bado wanahitajika kwa kiasi kikubwa.

Alieleza kuwa licha ya serikali kuweka mikakati maalum na kuyapa kipaumbele masomo ya sayansi kwa kuwashajiisha wanafunzi kuyasoma kwa bidii na hatimaye kujiendeleza katika vyuo vyake vitatu vikuu vilivyopo. Aliongeza kuwa lengo la kufanya hivyo ni kuwapata walimu na wataalamu wa masomo ya sayansi ili kuondokana na upungufu uliopo, ambapo tayari hata hivyo zipo nchi zinazosaidia kwa kuleta walimu wa masomo ya sayansi ikiwamo Nigeria.

Sambamba na hayo, Rais Dk. Shein alieleza uhaba wa madaktari wa upasuaji ambao bado wanahitajika katika kuimarisha sekta ya afya hapa nchini licha ya juhudi zinazochukuliwa na serikali za kuwasomesha wataalamu wa kada hiyo.

Naye Mratibu Mkuu wa programu ya kujitolea ya Umoja wa Mataifa (UNV), Oliver Adam, alimweleza Rais Shein azima ya propramu hiyo katika kuiunga mkono Zanzibar kuendeleza shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mratibu Mkuu huyo alimwakikishia Dk. Shein kuwa UNV iko tayari kushirikiana na Zanzibar katika kuhakikisha shughuli zote za kujitolea zinazosimamiwa na Umoja wa Mataifa (UN) na Zanzibar nayo itafaidika.

Aidha, Mratibu Mkuu huyo alieleza azima ya UNV ya kusaidia kuendeleza miradi kadhaa Zanzibar sambamba na kuzifanyia kazi hoja za Rais Dk. Shein za kuwawezesha vijana, kuimarisha sekta ya afya kwa kuongeza uwezo kwa madaktari wa upasuaji pamoja na walimu wa masomo ya sayansi na nyinginezo.

# Bodi yajitosa kutoa elimu kazi za kitaalamu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BODI ya Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majenzi Zanzibar, imesema kuwa utoaji wa mafunzo kwa wataalamu wake kutawajengea uwezo na uelewa wa kinachohitajika wakati wa maombi ya kazi za kishauri pamoja na mikataba inayotumika kwenye kazi hizo.

Akifungua mafunzo kuhusu manunuzi kwa watendaji hao, Mjumbe wa Bodi hiyo Mhandisi Ramadhan Mussa Bakari, alisema hatua hiyo pia itasaidia kuwajenga uwezo na kuingia katika ushindani wa masoko.

Alisema kuwa wataalamu hao wanahitaji kujua sheria za manunuzi ili kuweza kutimiza masharti na vigezo vinavyohitajika wakati wa kuomba kazi hizo za kitaalamu.

Alisema bodi imefikia maamuzi ya kutayarisha mafunzo hayo baada ya kuona kampuni za kiushauri Zanzibar ni kidogo na zilizokuwako hazipati kazi inavyotakiwa kwa sababu mbalimbali. Alizitaja baadhi ya sababu hizo ni kutotimiza masharti na vigezo vinavyohitajika wakati wa maombi na badala yake kazi hizo huchukuliwa na wataalamu kutoka nje ikiwamo China.

"Hapa tumeona wataalamu wetu wanakosa hamasa na kutojiamini katika kufungua kampuni za ushauri na kuingia katika ushindani wa kazi za kiushauri zinazoendana na taaluma zenu," alisema.

Aidha, alisema mafunzo hayo yamekuja muda mwafaka ambapo kazi za ujenzi zinazidi kuongezeka na sheria za manunuzi zinatoa fursa kwa Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla kupewa kipaumbele katika upatikanaji wa kazi za ushauri.

Aliwataka wataalamu hao kufafanua miongozo na fursa ambazo watoa huduma za ujenzi wamepewa ili iwe ni chachu ya kuingia katika ushindani wa kazi za kiushauri badala ya kuwaachia wageni kufanya kazi hizo.

Naye Mrajisi wa Bodi hiyo, Hawa Khamis Mzee, alisema mafunzo hayo yamekuja baada ya kugundua kuwapo tatizo katika masuala ya manunuzi ili kuwawezesha kufanya vizuri katika kazi zao.

# Museveni ataja sababu kukutana na maadui wa Kagame

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amevunja ukimya kuhusu madai ya kukutana na mfanyabiashara raia wa Rwanda, Tribert Rujugiro Ayabatwa, ambaye inaelezwa ndiye chanzo cha mvutano kati ya mataifa hayo mawili jirani.

Kupitia barua aliyomwandikia Rais wa Rwanda, Paul Kagame, Machi 10 mwaka huu na kuchapishwa katika Gazeti la serikali New Vision, Rais Museveni ameelezea mazingira aliyokutana na mfanyabiashara huyo ambaye Rwanda inasema yeye na wengine ni waasi wanaopanga kuiangusha serikali yake.

Katika barua hiyo, Rais Museveni alimwambia Rais Kagame kuwa alikataa kutoa uungwaji mkono kwa mfanyabiashara huyo, ambaye alikuwa anamwelezea mambo ya ndani ya Rwanda.

Aidha, Museveni alieleza kuwa alikutana na mfanyabiashara mwingine wa Rwanda, Charlotte Mukankusi ambaye alimwomba msaada baada ya kudai kuwa serikali ya Rais Kagame ilikuwa imemuua mume wake.

Wachambuzi wa siasa wameeleza kuwa barua hiyo inaonyesha kuwa kuna zaidi ya mvutano wa masuala ya kibiashara wakati huu ufumbuzi ukiwa bado haujapatikana dhidi ya mataifa hayo mawili.

Serikali ya Rwanda imekuwa ikiishtumu Uganda kwa kuwapa hifadhi na kuwaunga mkono wafuasi wa vuguvugu la RNC, ambalo Kigali inasema ni maadui wa serikali.

*RFI*

**Kupitia barua aliyomwandikia Rais wa Rwanda, Paul Kagame, Machi 10 mwaka huu na kuchapishwa katika Gazeti la serikali New Vision, Rais Museveni ameelezea mazingira aliyokutana na mfanyabiashara huyo ambaye Rwanda inasema yeye na wengine ni waasi wanaopanga kuiangusha serikali yake.**

# Misaada yapelekwa maeneo yaliyoathirika na kimbunga

**MAPUTO, Msumbiji**

NCHI za Msumbiji, Zimbabwe na Malawi, zimeanza kupokea misaada kutoka nchi mbalimbali, baada ya kuathiriwa vibaya na mafuriko yaliyoambatana na kimbunga Idai.

Kazi ya kufikisha misaada ilianza jana, lakini ilikuwa ngumu kwa sababu miundombinu muhimu kama viwanjwa vya ndege imeharibika vibaya.

Taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Shirika la Msalaba Mwekundu Msumbiji, Caroline Haga, ilieleza kuwa wahisani wengi hivi sasa wamezidisha mara mbili au tatu kiwango cha msaada walichokuwa wameahidi awali.

Umoja wa Ulaya (EU) umetenga Dola za Marekani milioni nne kwa ajili ya msaada wa dharura, Uingereza imeidhinisha dola milioni nane, na Tanzania imepeleka tani 238 za msaada wa chakula na dawa, zikibebwa na ndege zake za kijeshi. Idadi ya watu ambao wamethibitika kuuawa na kimbunga Idai imekwishafika 300, hizo zikiwa takwimu za Msumbiji na Zimbabwe tu, na idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka mara tatu zaidi ya hiyo ya sasa.

Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, alisema watu 350,000 nchini mwake wanakabiliwa na kitisho kikubwa, na ametangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa kwa ajili ya waliouawa na kimbunga Idai.

Watu wanaofanya kazi ya kuokoa wanatumia mitumbwi na helikopta kuwatafuta manusura waliojihifadhi juu ya paa za nyumba na kwenye matawi ya miti.

Shirika liitwalo Rescue South Africa limesema tangu Ijumaa iliyopita siku ambayo kimbunga hicho kilitokea limeshawaokoa watu 34 kwa kutumia helikopta.

Nchini Zimbabwe, Rais Emmerson Mnangagwa alitembelea eneo la Chimanimani lililokumbwa na mafuriko mabaya, na kusema kuwa nchi jirani zinazoizunguka Zimbabwe zinataka kutoa usaidizi.

"Nchi kama Afrika Kusini, Botswana, Namibia na Angola zimetaka kujua msaada tunaouhitaji, na tuko mbioni kuorodhesha vitu vinavyohitajika, ambavyo tunaamini wanaweza kutusaidia kuvipata," alisema Rais Manangagwa.

Mashirika ya kimataifa nayo yamewasili, likiwamo lile la Umoja wa Mataifa linalosaidia chakula WFP ambalo limeahidi kuwasaidia watu kati ya 500,000 na 600,000.

Msemaji wa shirika hilo, Herve Verhoosel, aliwaambia waandishi wa habari mjini Geneva, kwamba nchi nyingi duniani bado hazijatambua ukubwa wa matatizo katika ukanda wa Kusini Mashariki mwa Afrika.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuratibu Msaada wa Kibinadamu (OCHA) tayari linasaidia kukusanya taarifa na kuzishughulikia, wakati Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) likisambaza vifaa muhimu kama mahema, majisafi na vifaa vya shule kwa watoto.

*DW*



Jeshi la Msumbiji likigawa msaada wa chakula kwa wananchi wa nchi hiyo, ambao wameathirika na mafuriko pamoja na kimbunga. **PICHA: ALLIANCE**

# Marekani yalaumiwa kuua raia Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

JESHI la Marekani linaloendesha mashambulizi ya angani nchini Somalia dhidi ya ngome za wapiganaji wa Al Shabab limelaumiwa kwa madai ya kuwaua raia katika mashambulizi hayo.

Shirika la Umoja wa Mataifa linalotetea haki za binadamu la Amnesty International limesema kuwa katika mashambulizi matano iliochunguza watu 14 waliuawa na wengine saba kujeruhiwa.

Hata hivyo, Marekani imekana kwamba hakuna raia waliouawa katika operesheni hizo mbili.

Taarifa kutoka kwa Ofisa wa Shirika la Amnesty International, Seif Magango, ilieleza kuwa mashambulizi hayo yaliwalenga raia wasio na hatia ambao walikuwa wakiendelea na shughuli za kawaida na ambao hawakuwa na uhusiano wowote na kundi la Al-Shabab.

Magango alisema kuwa mashambulizi hayo yalifanyika katika Jimbo la Lower Shebelle katika mitaa kadhaa ikiwamo Faraweis, na Ilimei.

Katika mtaa wa Faraweis watu saba waliuawa ikiwamo wanawake na watoto, huku wakulima watatu waliokuwa wakiendelea na shughuli zao za kilimo wakipigwa kombora na kuuawa papo hapo.

Ofisa huyo alisema kuwa hali hiyo ilianza tangu Rais wa Marekani, Donald Trump, kutangaza kuwa jeshi lake litakuwa likitumia ndege zisizokuwa na rubani kukabiliana na wapiganaji hao katika eneo hilo linalodaiwa kuwa na vita.

"Tangu Rais Trump aingie madarakani kumekuwa na mashambulizi zaidi ya 100 na tunachouliza ni kwamba je, ni watu wangapi watakaouawa itakapofika mwisho wa mwaka huu," alisema Magambo.

Lakini saa chache tu baada ya kutoa ripoti hiyo, Jeshi la Marekani limetoa taarifa yake likikanusha habari hizo na kusema kwamba kikosi cha AFRICOM kinazuia mauaji ya raia wasio na hatia wakati wa mashambulizi yake dhidi ya kundi la wapiganaji wa Al-Shabab.

Katika taarifa hiyo AFRICOM ilieleza kuwa lengo la mashambulizi yake ni kuwalinda raia wa Somalia dhidi ya ugaidi mbali na kuisaidia serikali ya Somalia kukabiliana na changamoto za kiusalama.

"Amnesty International ilitoa ripoti ikidai kwamba mashambulizi nane ya AFRICOM kati ya mwaka 2017 na 2018 yalisababisha vifo vya raia. Tunashukuru juhudi za Amnesty International kuturuhusu kuchangia katika ripoti hiyo kabla ya uchapishaji wake licha ya kwamba tunaamini kwamba sio ya ukweli," ilieleza taarifa hiyo na kuongeza.

"Tumechukulia madai ya mauaji ya raia kwa uzito mkubwa bila kutazama wanakotoka. Wakati wa utafiti wa ripoti yake, Shirika la Amnesty International liliwasilisha madai 13 dhidi yetu mnamo Oktoba 2018 na Februari 2019.

"Uchunguzi wetu ulibaini kwamba hakuna shambulio hata moja la AFRICOM lililosababisha maafa ama majeruhi. Uchunguzi wetu ulihusisha mbinu za kijasusi ambazo haziwezi kutumiwa na mashirika yasiokuwa ya kijeshi."

*BBC*

# Mradi nyumba 10 kupunguza adha ya watumishi Muheza

**Na Steven William, MUHEZA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, inajenga nyumba 10 kwa ajili ya watumishi ambazo zitasaidia kupunguza tatizo la kukaa mbali na kituo cha kazi. Nyumba hizo za gharama nafuu zinajengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika eneo la Chatur, katika kijiji cha Kibanda.

Akitoa taarifa juzi ya ujenzi wa nyumba hizo kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ambaye aliongozana na Naibu wake, Angeline Mabula na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Maulid Banyani, alisema shirika linajenga nyumba ikiwa sehemu ya mipango yake ya uendelezaji miliki.

Banyani alisema shirika lilipokea maombi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya kujengewa nyumba za makazi na lilianzisha mradi unaohusisha usanifu na ujenzi wa nyumba 20 za makazi ya gharama nafuu na 10 kati ya hizo ni za halmashauri hiyo.

Alisema mkataba wa uendelezaji wa mradi huo, ulitiwa saini Septemba 29, 2017 na ulikamilika ndani ya mwaka mmoja kuanzia tarehe ya malipo ya kwanza ya Sh. 117,092,580.

Banyani alisema kuwa gharama za uendelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huo umekadiriwa kuwa Sh. 657,221,635.00 bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Alisema halmashauri inanunua nyumba hizo kwa Sh. 390,308,600 bila ya VAT.

Mkurugenzi huyo wa NHC alisema hadi mwezi huu, gharama iliyotumika katika ujenzi huo ni Sh. 273,745,774. 91 bila VAT.

Waziri Lukuvi alishauri taasisi binafsi, mashirika ya serikali na watu binafsi kuitumia Taifa NHC katika ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa kuwa wana mafundi wazoefu na gharama zao ni ndogo kulinganisha na kampuni zingine.

Alisema NHC inatekeleza mpango mkakati wake wa miaka 10 wa mwaka 2015/2016 hadi 2024/2025 kwa kuwezesha kupata nyumba bora za gharama nafuu nchini.

Kupitia mpango mkakati huo, alisema NHC inalenga kujenga nyumba 30,000 nchini sawa na asilimia 40 ya mpango mzima.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, pamoja na viongozi hao wa wizara, walitembelea ujenzi wa nyumba 10 na kuridhika na maendeleo ya mradi huo.

# Wabunge wa Chadema kutetea mahabusi, wafungwa mjengoni

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimewaelekeza wabunge wake wasimame kidete kwenye kikao kijacho cha Bunge la Bajeti kuhakikisha wanatetea haki na maslahi ya askari Magereza, mahabusi na wafungwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, (Zanzibar), Salum Mwalimu, alisema maamuzi hayo yametokana na kikao cha sekretarieti ya chama walichokaa.

"Sekretarieti ya chama imekaa na kujadili kwa kina hatua nyingine za ziada ambazo zitakazia yale aliyosema Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe, wiki iliyopita kuhusu changamoto zilizopo magerezani," alisema.

Mwalimu alisema katika kikao hicho, wamependekeza mambo mawili ambayo wabunge hao wanatakiwa kuyafanya kuwa ni kutetea haki na maslahi ya kundi hilo pamoja na kuzipitia sheria ambazo zinanyima haki hizo ili ziweze kubadilishwa.

"Kama mtakumbuka wiki iliyopita Mbowe pamoja na Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko, walieleza maisha waliyoyaona gerezani ndani ya siku 104 walizokaa Segerea, jijini Dar es Salaam," alisema.

Alisema miongoni mwa yaliyoelezwa siku hiyo ni pamoja na kuwapo kwa mrundikano wa mahabusi unaosababishwa na upelelezi na uchunguzi wa kesi zao kutokamilika kwa wakati na kuwapo kwa ugonjwa wa ngozi maarufu kama burudani.

Mwalimu alisema kutokana na changamoto hiyo, Mbowe aliomba ofisi ya Jaji Mkuu, Jeshi la Polisi na Kamishna wa Magereza, wafanye operesheni ya kusafisha Magereza.

Pia alidai lipo tukio la mfanyabiashara Mussa Adam, ambaye baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi walimbambika kesi ya mauaji huko Tabora na kusababisha Rais Magufuli kuielekeza ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), alifuatilie.

"Tumeona ofisi ya DPP imetuma watu ndani ya muda mfupi kwenda kulifuatilia na ukweli ukabainika na shtaka la mauaji alilopewa likafutwa, tumeona Jeshi la Polisi wametuma mtu kufuatilia nini kimetokea," alisema.

Mwalimu alisema mambo hayo mawili yanaonyesha na kuthibitisha aliyozungumza Mbowe kuhusu makandokando mengi ya upatikanaji wa haki.

"Huyu kijana asingekuwa na ujasiri wa kuandika alichoandika na kama Rais Magufuli asingekuwa na muda wa kuyasoma maana yake leo angekuwa gerezani akituhumiwa kwa kosa la mauaji," alisema.

Aliongeza: "Angeishi gerezani miaka nenda rudi kwa kile ambacho Mwenyekiti Mbowe alikieleza wiki iliyopita kuwa, kivuli kinachotumiwa na Jeshi la Polisi na ofisi ya DPP kwenye kesi ni upelelezi unaendelea, huu ni mfano ulio hai kabisa huyu kijana kaonewa na Jeshi la Polisi limekiri na linachukua hatua," alisema.

Alisema ni lazima rai iliyotolewa na Mbowe kuwa iundwe tume au kamisheni maalum kwenda kupitia majalada ya waliopo magerezani ili wasio na hatia watendewe haki na upelelezi ukamilike, iundwe tume na kuanza kazi.

Akizungumzia kuhusu kitendo cha Maalim Seif Sharif Hamad cha kuhamia ACT-Wazalendo, Mwalimu alisema kama angehamia Chama Cha Mapinduzi (CCM), ingeleta taharuki na mshangao mkubwa.

Alisema Chadema inaamini alichokifanya Maalim Seif, kimelenga maslahi mapana ya mabadiliko Tanzania Bara na Visiwani, kuliko maslahi yake binafsi wala chama chochote.

"Angekwenda kwingine pengine hatari ingekuwa kubwa zaidi, lakini aliko bado tunaendelea kushirikiana naye ili kuimarika zaidi badala ya kubomoka zaidi," alisema.

Aliongeza: "Maalim Seif bado yumo mule mule kama ni familia unaweza kusema ni mtoto wa baba mdogo na mkubwa, sioni tatizo lolote bado anacheza kwenye laini ya vyama vile vile vilivyokuwa kwenye mazungumzo na ushirikiano bungeni na nje ya Bunge," alisema.




Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Dk. Raphael Chegeni (kushoto), akizungumza na wanahabari baada ya kamati yake kufanya ziara kutembelea miradi inayoendeshwa na kusimamiwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya TTCL, Mhandisi Omari Rashid Nundu na Mkurugenzi Mkuu wa TTCL Corporation, Waziri Waziri Kindamba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vigogo kortini tuhuma ufisadi bil. 9.1/-

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Mara, imewafikisha mahakamani watuhumiwa watatu akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (Muwasa), Hawaiju Gantala.

Watuhumiwa hao wamefikishwa mahakamani hapo kujibu tuhuma za kesi ya kuhujumu uchumi na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 9.13.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mkurugenzi wa Nyakirang'anyi Construction Company Limited, Mahuza Nyakirang'anyi, ambaye alikuwa mkandarasi katika mradi huo na aliyewahi kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Muwasa, Emmanuel Ruyobya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Naibu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mara, Daniel Kapakala, watuhumiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mara mjini Musoma kwa makosa mbalimbali ya rushwa wanayodaiwa kutenda wakati wa utekelezaji wa mradi wa maji Bunda ambao serikali ilitoa Sh. 9,130,446,846.99.

"Mashtaka hayo ni pamoja na kula njama na kuisababishia mamlaka upotevu wa Sh. 613,500,000," taarifa ilieleza.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, shtaka la pili linamhusu Gantala, anayedaiwa kuwa Januari 18, 2017, aliandaa hati ya kukamilisha kazi (Certificate of Completion) iliyolenga kumlipa Nyakirang'anyi Sh. 7,547,348,246 huku akijua mkandarasi huyo hakuwa amemaliza kazi aliyopewa kwa mujibu wa mkataba jambo ambalo ni hujuma kwa mamlaka.

Ilisema Gantala, anashtakiwa kwa tuhuma za kutumia nyaraka za uongo kwa lengo la kumdanganya mwajiri wake kinyume cha kifungu cha 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

Katika shtaka hilo, anadaiwa Januari 18, 2017 aliandaa hati ya kukamilisha kazi (Certificate of Completion) huku akijua kuwa mkandarasi Nyakirang'anyi hajakamilisha mradi huo kwa mujibu wa mkataba na huku akifahamu kuwa yaliyoandikwa katika hati hiyo hayakuwa ya kweli.

Katika shtaka la nne washtakiwa wote watatu wanadaiwa kutakatisha fedha kiasi cha Sh. 613,500,000 kinyume cha kifungu cha 12(d) na 13(a) cha Sheria ya Kuzuia Utakatishaji Fedha namba 12 ya mwaka 2006.

Katika shtaka la tano, washtakiwa wote watatu wanashtakiwa kwa uhujumu uchumi na kuisababishia mamlaka hasara ya Sh. 613,500,000 kinyume cha aya ya 10(1) ya jedwali la kwanza na kifungu cha 57(1) na 60(2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi sura ya 200.

Washtakiwa wamerudishwa rumande hadi Aprili 3, mwaka huu, kwa kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mara bado haijateuliwa kusikiliza shauri hilo.

Ilielezwa kuwa washtakiwa wawili wanatafutwa ili kufikishwa mahakamani kwa makosa hayo ambao ni Juvenary Shilianga, Mkurugenzi wa Kampuni Fotress Building na Peter Kisobare ambaye alikuwa Mhandisi wa Muwasa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**WAFANYAKAZI WA HOTELINI**, Wanatakiwa wafanyakazi wa Usafi, Wahudumu, Wapishi na Meneja. Bagamoyo mjini, wawe na vyeti na uwezo wa kuongea Kingereza. kwa Mawasiliano piga namba: 023-2440004/0657, 233970/0768 296667


**NAFASI ZA KAZI UALIMU / CERTIFICATE** au diploma / english/mathematics na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## VYETI VIMEPOTEA



**YOHANA ZACHARIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2508-0046 kilichotolewa na ISENI SEKONDARI Mwaka 2009. Cheti cha Diploma chenye namba **OD/2012/WS 94** kilichotolewa na Chuo cha Maji Dar mwaka 2015. Cheti cha kuzaliwa namba **1344625** kilichotolewa mwaka 2012. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MW/RB/8549/2018.**

115128702

## CHETI KIMEPOTEA



**HASSANI ALLY YASINI wa KONGWA,** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuzaliwa ambapo namba ya usajili haikumbuki , kilichotolewa Ofisi ya Vizazi na Vifo Tanzania.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: KNG/RB/339/2019.**

215128002

## CHETI KIMEPOTEA



**TIMILO ATHUMANI HASSANI wa KONGWA,** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuzaliwa ambapo namba ya usajili haikumbuki , kilichotolewa Ofisi ya Vizazi na Vifo Tanzania.

Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.
taarifa ya polisi:
**KNG/RB/340/2019.**

215127902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JULIUS MUGISHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 243 DAU SUBARU - LEGACY.** Chassis namba **BP5100642.** Engine namba **EJ20C676311** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/3396/2019.**

115128902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENO MORRI MALISA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T **915 APQ NISSAN PATROL.** Chassis namba **ICS5BJPC855903348.** Engine namba **P60325.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **OB/RB/2683/2019.**

115128802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MOHAMED MBARAKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 853 AER TOYOTA HILUX.** Chassis namba **LN1060013874.** Engine namba **3L1918642.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **BAG/RB/1008/2019.**

115129002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALLY HUSSEIN NINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 904 CBT** AINA YA **SCANIA.** Chassis namba Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifayapolisi: **KJN/RB/1521/**

XXXXXXX

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**BERTHA HEZRON LUZABIKO** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari **NISSAN PATRON** yenye namba za usajili T972 ADX Chassis no. **JNITESY6120520713,** Engine no. **ZD30047176**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi.

Taarifa ya polisi: **CD/IR/RB/1731/2019**

115128102

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ONESMO BAHARIA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC 882 ACH. Chassis namba MD2A21BZ6EWE68. Engine namba **PFZWEE16421.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/347/2019.**

115128302

**IN THE DELEGATE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 22 OF 2019**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**VICENT ELISHA MSAMBAZI**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY EGLA WILLIAM KUTIMWA**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased s estate are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of petition for letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections (if any) to the grant should be filed on or before **Day of 5th APRIL, 2019.**

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

**Dated 20th This day of March, 2019.**

215128402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 20/03/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe 22/03/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka ARUSHA kuelekea DAR- ES- SALAAM gari hilo lenye namba za usajili: **T748, BBW T891 ANB,T567CZX,T750 CUU.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 24
   Upana –mita 3.7
   Kimo – mita 4.6
3. Njia itakayotumika **ARUSHA** hadi **DAR-ES-SALAAM kupitia BAGAMOYO** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215128602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 20/03/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **22-03-2019** kampuni ya **M.M CORP LTD** tasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa.
2. Kutoka Kibaha kuelekea **MKURANGA** gari hilo zenye namba za usajili:
   **T898 APY HORSE/ T933 AFZ**

   Gari hilo linavipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 22.00
   Upana -mita 3.50
   Kimo -mita 48.00
3. Njia itakayotumika Kibaha hadi Mkuranga Kupitia Kilwa road.
   Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaombaradhikwausumbufuutakaojitokeza.**

115127002

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**SALVATORY NICOLAUSI HAMARO** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki FEKON yenye namba za usajili T.341 CTJ Chassis n.o LDAPnJOBXDGB22338, Engine no.157FMI213122338

Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi: **URP/RB/1512/2019**

215127702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBA: 17.. 2018**
**MSIMAMIZI: RAFIA AMBWENE NA AWADHI RASHID SHEHOZA**
**DHIDI YA**
**MAREHEMU: RASHID HEMED SHEHOZA**

**Kwa: AWADHI HEMED SHEHOZA**

**Ombi la Mdai/MSIMAMIZI:**
**RAFIA AMBWENE MWAKISWAGA**
**Madai ya: MIRATHI**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 25 mwezi 03 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 19 mwezi 03 mwaka 2019.

115129102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 56.. 2019**
**Mdai: SALOME SAIMON MBIRO**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: JOYCE LEONARD MABULA**

**Kwa: JOYCE LEONARD**
**GEITA**

**Ombi la Mdai: SALOME SAIMON MBIRO**
**Madai ya: PESA SHILINGI 850,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 7 mwezi 03 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 25 mwezi 02 mwaka 2019.

115129202


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MOURINHO ATANGAZA KURUDI RASMI KAZINI

**LONDON, England**

JOSE Mourinho ametangaza mpango wake wa kutaka kurudi kwenye kazi ya ukocha kipindi cha majira ya joto baada ya kuzipiga chini ofa tatu.

Raia huyo wa Ureno hajawa na timu yoyote tangu alipofukuzwa pale Manchester United Desemba mwaka jana, baada ya kukaa kipindi cha miaka miwili na nusu hapo kwa 'Mashetani Wekundu' hao.

Hata hivyo, beIN Sports imeeleza kocha huyo wa zamani wa Chelsea amekuwa akipewa nafasi kadhaa, lakini bado anasubiri ile anayoitaka yeye.

Wakati alipoulizwa kuhusu majaliwa yake, Mourinho alisema: "Ni miezi mitatu na nusu sasa tangu nilipokuwa kocha wa timu na sasa najiandaa tena kurudi kwenye kazi hiyo.

"Wakati unapokuwa kwenye soka la dunia, lazima uendelee kuwa kwenye maisha yale uliyoyazoea.

"Nafasi ya ukocha ni maalum kwa ajili ya kuifurahia kila siku. Nataka kurudi kwenye nafasi yangu ya ukocha kipindi cha majira ya joto, kuanzia Juni mwanzoni mwa msimu ujao.

"Najua kabisa nini ninachotaka, kwa kuwa tayari nimeshazikataa ofa tatu za kuwa kocha. Na pia najua nini ninachotaka.

"Simaanishi jina la timu, lakini aina ya kazi na staili ya klabu husika. Najua nini ninachokitaka na natumaini kukipata."





# GRIEZMANN
## AZUA VITA MAN UNITED, BAYERN

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeingia kwenye vita za mbio moja na Bayern Munich katika kuwania saini ya nyota wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa majaliwa yake hapo kwenye mji mkuu wa Hispania yapo shakani, huku taarifa zikieleza kwamba, anataka kuondoka katika timu hiyo.

Griezmann awali alikubali kubakia na Atletico badala ya kujiunga na Barcelona kipindi cha majira ya joto, lakini sasa majaliwa yake yapo shakani.

Lakini taarifa za hivi karibuni zinaeleza kwamba, kuna uwezekano mkubwa wa nyota huyo kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

United imeingia kwenye mbio za kutaka kumsajili mshindi huyo wa Kombe la Dunia kwa ajili ya kuziba pengo la Alexis Sanchez ambaye naye anaonekana ni wazi kwamba ataondoka mwishoni mwa msimu.

Wakati huo huo, Bayern imepanga kumsajili Griezmann kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chake.

Rais wa Bayern, Uli Hoeness, mapema wiki hii aliahidi kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chake hicho ili kuwa na wakati mzuri zaidi msimu ujao.

"Tupo kwenye mchakato wa kuiimarisha timu yetu. Kwa sasa huu ndio uwekezaji wetu mkubwa na tutaka kufanya usajili wa wachezaji wakubwa," alisema rais huyo wa Bayern.

# De Ligt akaribia kutua Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

NAHODHA wa Ajax, Matthijs de Ligt, anakaribia kutua Klabu ya Barcelona baada ya miamba hao kutoa ofa ya awali ya euro milioni 60.

Beki huyo chipukizi, ambaye ni mmoja wa wachezaji wanaotarajiwa kung'ara zaidi Ulaya, amekuwa akihusishwa zaidi na mpango wa kumfuata mchezaji mwenzake wa Ajax, Frenkie de Jong ambaye atahamia Barcelona kipindi kijacho cha majira ya joto.

Licha ya kwamba walishindwa kufikia makubaliano Novemba mwaka jana, lakini Gazeti la Marca limeripoti kwamba, Barcelona wametuma ofa ya euro milioni 60 kwa ajili ya kumsajili beki huyo kipindi cha majira ya joto.

Gazeti la AS limeripoti kwamba Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amebainisha kwamba yupo tayari kuhakikisha mchezaji huyo anatua kwa miamba hao.


Barcelona inataka kupata mrithi wa mkongwe Gerard Pique ambaye kwa sasa anakaribia kustaafu, huku Samuel Umtiti akiwa ameshindwa kuonyesha kipaji chake kutokana na kusumbuliwa na majeraha.

Na inaonekana wazi kwamba, Matthijs de Ligt atafuata nyayo za mwenzake, Frenkie de Jong, ambaye tayari ameshamalizana na Barcelona ambapo atajiunga nao kipindi cha majira ya joto.



# BILIONEA

## ALIYEMZIDI UTAJIRI ABRAMOVICH KUINUNUA CHELSEA



**LONDON, England**

BILIONEA wa Uingereza, Sir Jim Ratcliffe bado ameendelea kuonyesha kutaka kuinunua klabu ya Chelsea, huku nia hiyo ikionekana kugonga mwamba mbele ya mmiliki wa timu hiyo, Roman Abramovich kutokana na dau dogo aliloweka mezani.

Kwa mujibu wa vyombo mbalimbali vya habari, Ratcliffe mwaka jana alitoa ofa kwa miamba hiyo ya Ligi Kuu ya England, lakini bado dili hilo halijakamilika.

Ratcliffe ambaye anakadiriwa kuwa na utajiri wa pauni bilioni 21, hivi karibuni anatarajiwa kuwa mmiliki wa timu ya Baiskeli ya Team Sky kabla ya kuinunua na Chelsea.

Hata kama, Abramovich hajachukulia kwa umakini mkubwa dhamira ya bilionea huyo wa Kiingereza, dau analotaka yeye ni pauni bilioni 2.1.

Abramovich amekosekana katika dimba la Stamford Bridge karibia msimu mzima kufuatia wakati mgumu anaopitia kwa sasa wa kunyimwa visa kutokana na mambo ya kimahusiano baina ya Uingereza na Urusi.

Hata hivyo, mmiliki huyo anafahamu kuwa na pasipoti ya Israeli, huenda ikamruhusu kutua Uingereza pasipo visa.

Abramovich pia anampango wa kuuboresha Uwanja wa Stamford Bridge na kuuongeza uwezo wa kuingiza mashabiki kutoka idadi ya watu 41,631 na kufikia 63,000 ifikapo msimu wa mwaka 2023/24.

Hata hivyo, kutokana na maboresho ni ishara tosha kuwa Chelsea haiwezi kuuzwa kwa sasa.

Ratcliffe anaifuatilia Chelsea kwa sababu ni karibu na nyumbani kwake anapokaa.

Kwa mujibu wa Sunday Times ya mwaka 2018, ilitoa tofauti ya utajiri wa watu hawa wawili, ikieleza Ratcliffe anamiliki utajiri wa paundi bilioni 21.05, wakati Abramovich anamiliki utajiri wa pauni bilioni 9.3.

Wakati kampuni yake ya 'Ineos' inarekodi ya kuuza pauni bilioni 45 na kuwa na jumla ya wafanyakazi zaidi ya 18,500 kutoka nchi 22.



# Ibrahimovic: Ferguson ameidumaza Man United

**NEW YORK, Marekani**

ALIYEKUWA mshambuliaji wa Manchester United ambaye kwa sasa anaichezea Galaxy ya nchini Marekani, Zlatan Ibrahimovic, amefunguka na kumtupia lawama aliyekuwa kocha wa Manchester United, Sir Alex Ferguson kutokana na maendeleo ya timu hiyo.

Ibrahimovic amesema Ferguson ndiye anayezuia maendeleo ya klabu hiyo, kutokana na mafanikio yake ya awali.

United imeshindwa kutwaa taji la Ligi Kuu tangu kustaafu kwa kocha huyo raia wa Scotland mwaka 2013.

Jose Mourinho alikuwa kocha wa kudumu wa tatu kuondoka kushindwa kukidhi matarajio huko Old Trafford, na Ole Gunnar Solskjaer akiinua katika miezi ya hivi karibuni kama kocha wa muda mfupi.

Lakini Ibrahimovic, aliyeitumikia United zaidi ya miezi 18, ikiwa ni pamoja na mabao 28 katika msimu wake wa kwanza, anasisitiza kulinganisha na mafanikio yaliyomo chini ya Sir Alex wamezuia klabu hiyo kuendelea.

"Kila kitu kinachotokea kinahukumiwa na zama za Ferguson," Ibrahimovic alisema akiliambia Gazeti la The Mirror.

"Wanasema eti laiti Ferguson angekuwapo hapa, hali hii isingeweza kutokea, Ferguson hakutaka kufanya hivyo kama hiyo. Ferguson angefanya hivyo kama hii. Kila kitu kilikuwa Ferguson.

"Ikiwa ni mimi, ningesema simjui Ferguson tena. Na mimi kuja hapa na nataka kufanya historia yangu mwenyewe, nataka kufanya hadithi yangu mwenyewe.

"Kwa hivyo sitaki kusikia kilichotokea hapo awali. Ninataka kufanya hivyo kwa sasa nakuja na mawazo mapya. Ferguson ana nafasi yake katika historia katika klabu hii lakini sasa klabu inaendelea. Inapaswa kupata utambulisho wake na ni vigumu. "

# KROOS KUMRITHI RABIOT PSG

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya PSG imehamishia nguvu zao kumwania nyota wa Real Madrid, Toni Kroos, wakati wakitaka kuziba pengo la Adrien Rabiot, ambaye anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo kipindi cha majira ya joto kijacho.

Kroos amekuwa na msimu mbaya pale Madrid na PSG inaonekana kuwa tayari kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, huku wakitaka kuimarisha kikosi chao baada ya kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. Kwa mujibu wa OKDiario, miamba hao wa Ufaransa wapo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 68 kwa ajili ya kiungo huyo wa zamani wa Bayern Munich.

Huku majaliwa ya baadaye ya Rabiot yakioneana kutokuwa sawa pale PSG, na kuna uwezekano mkubwa wa kufunguliwa milango yake wakati wa kipindi kijacho cha majira ya joto.

Habari kutoka ndani ya Real Madrid zinaeleza kwamba, Kroos mwenyewe yupo tayari kuondoka kwenye klabu hiyo na licha ya ujio wa kocha mpya, Zinedine Zidane.

Kroos alikuwa mchezaji muhimu wa Madrid wakati walipotwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo chini ya Zidane.



## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SANCHEZ ATOA MSIMAMO HATIMA YAKE MAN UNITED

**Manchester, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez, ameamua kuweka kando mwaka wake wa kwanza mgumu katika klabu hiyo na kudhamiria kulipa mafanikio kwa mashabiki wa miamba hiyo ya Old Trafford.

Nyota huyo wa kimataifa wa Chile anapitia katika kipindi kigumu Old Trafford tangu alipojiunga nayo akitokea Arsenal Januari mwaka jana, na kushuhudiwa Henrikh Mkhitaryan akitua Emirates.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amefunga mabao matatu tu katika mechi 29 za Ligi Kuu alizocheza, na amekuwa akihaha kurejea katika kiwango chake chini ya Jose Mourinho na sasa chini ya kocha wa muda Ole Gunnar Solskjaer, na hivyo kusababisha tetesi kuwa United tayari inapanga kumfungulia mlango wa kutokea mchezaji huyo anayeripotiwa kulipwa pauni 350,000 kwa wiki.

Sanchez kwa sasa anasumbuliwa na majeraha ya goti baada ya kuumia wakati wakishinda 3-2 dhidi ya Southampton mwezi huu na hatarajiwi kuwa fiti hadi takribani katikati ya Aprili, na kuzua mapendekezo kuwa angeweza kucheza mechi yake ya mwisho, lakini mshambuliaji huyo anataka kushinda kwa kuwapa mashabiki furaha.

"Ni wazi, ninataka kuwafanya mashabiki wa United kuwa wenye furaha," aliliambia Jarida la United kabla ya kuumia. "Ninataka kufunga mabao. Ninataka kuwapa furaha. Ninataka kushinda medali.

"Wakati tulipopoteza mechi ya fainali ya Kombe la FA mwaka jana dhidi ya Chelsea, sikuwa na furaha. Sikufurahi kwa ujumla. Ukweli, niliumia kwa sababu nilitaka kuwafanya mashabiki wetu wa kushangaza kwa kuwa na furaha. Niliona mashabiki walikuja kupaki nje ya Uwanja wa Wembley. Wote walinizunguka, wote wekundu. Nilipenda hili. Wembley yote ilikuwa nyekundu.

"Bao pale [Wembley] dhidi ya Tottenham liliingia akilini. Ulikuwa wakati mzuri sana kwa sababu mashabiki wa United walikuwa sahihi juu yetu na ulikuwa wakati mzuri wa kusherehekea pamoja nao.

"Wakati nilipokuwa mdogo, niliipenda United. Ninaapa. Kama mtoto mdogo, niliipenda United. Ukweli ninawapenda. Na ninataka kulionyesha hili na kuwaletea watu furaha kwa sababu, ni wazi, ninataka kushinda.

"Ninataka kuendelea kuonyesha mapenzi yangu kwa mpira. Ninajua nini ninachoweza kukifanya, nina imani ndani ya uwezo wangu. United ni klabu muhimu, na si England pekee bali katika ngazi ya dunia na ningependa kusaidia kuleta kombe kwa mashabiki."

Kiwango bora cha Sanchez alikipata akiwa na jezi ya Arsenal, ambapo alivutia kwa kuwa thabiti chini ya Arsene Wenger baada ya kujiunga na klabu hiyo akitokea Barcelona mwaka 2014.

Akiwa amezaliwa huko Tocopilla Kaskazini mwa Chile, Sanchez anakiri kamwe hakuwahi kufikiria angefurahia mafanikio ya kazi yake huko Ulaya.

"Mara zote ilikuwa ligi ya Chile kwangu, lakini safari yangu ya kisoka iliendelea na nilicheza Argentina na Italia, na baadaye, ilikuwa kama: 'Wow, hili ni soka! Napenda soka!'

## KWA UFUPI

**GRIEZMANN ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United inapewa nafasi zaidi ya kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid na mshindi wa Kombe la Dunia, Mfaransa Antoine Griezmann, 27, katika majira ya kiangazi. ***(Sport, via Manchester Evening News)***

**HAZARD HAIFIKIRII REAL MADRID**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Mbelgiji Eden Hazard, 28, amesema hatatibuliwa na tetesi zinazoendelea kuwa atajiunga na Real Madrid majira ya kiangazi. ***(Metro)***

**MANOLAS KUTUA UTD AU ARSENAL**

MANCHESTER United ama Arsenal inaweza kumpata beki wa kati wa Roma, Mgiriki Kostas Manolas, 27, kwa ada ya punguzo majira haya ya kiangazi. Dau la kuvunja mkataba la beki huyo litashuka kama timu yake haitafuzu michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Calciomercato, via Mirror)***

**COURTOIS, DE GEA HAWATAPISHANA**

REAL Madrid na Mbelgiji Thibaut Courtois, 26, wamekataa uwezekano wa kipa huyo kufanywa chambo katika mpango wa kuipata huduma ya kipa wa Manchester United, Mhispania David de Gea, 28. ***(Sun)***

**IBRAHIMOVIC AIANIKA CITY**

MSHAMBULIAJI wa Los Angeles Galaxy, Zlatan Ibrahimovic, 37, amefunguka kwa nini aliikataa Manchester City mwaka mmoja kabla ya kujiunga na wapinzani wao, Manchester United mwaka 2016. ***(Mirror)***

**DYBALA NI MUDA TU LIVER**

LIVERPOOL inaweza kuwa tayari kukubali dili la kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Paulo Dybala, 25, kutoka Juventus. ***(Tutto Mercato, via Team Talk)***

**KROOS AIVUTIA PSG**

PARIS ST-GERMAIN inavutiwa kumsajili kiungo wa Real Madrid, Toni Kroos, 29, na mabingwa hao wa Ufaransa wapo tayari kulipa pauni milioni 68.5 ili kumpata nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani. ***(OK Diario, via Sport)***

**UNITED YAFUNGULIWA RABIOT**

MANCHESTER United bado ina nafasi ya kumsajili kiungo wa Paris St-Germain, Adrien Rabiot, 23, baada ya mama yake, ambaye pia ni wakala wake, kukanusha taarifa kuwa nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa amekubali kujiunga na Barcelona. ***(L'Equipe, via Metro)***

**GIROUD KUIKIMBIZA MARSEILLE, LYON**

MSHAHARA anaotaka Olivier Giroud, 32, utamfanya mshambuliaji huyo wa Chelsea na Ufaransa kuwa ghali sana kwa Marseille ama Lyon. ***(Le10 Sport - in French)***

**WEST HAM, NEWCASTLE VITANI**


WEST HAM na Newcastle United zinamtupia jicho kiungo mshambuliaji wa Mainz, Erkan Eyibil, 17, Mturuki huyo anaelezwa kuwa 'Mesut Ozil' mpya. ***(Turkish Football)***

**KANE HATAKI MPASUKO ENGLAND**

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane, 25, amesema wachezaji wa kikosi hicho hawataruhusu upinzani wa klabu kusababisha mpasuko katika majukumu ya kimataifa. ***(Times)***

**ALVES KUJIFUNGA TENA PSG**

BEKI wa Paris St-Germain, Mbrazil Dani Alves, 35, amekubali kuongeza mkataba na mabingwa hao wa Ufaransa. ***(ESPN)***



## HABARI MICHEZO

# KIWANGO CHA MWAKINYO, ZARIKA GUMZO ENGLAND

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA nyota Mtanzania, Hassan Mwakinyo amewasili jijini, Nairobi Kenya salama na yuko tayari kwa pambano lake la kimataida dhidi ya Eduardo Gonzalez kutoka Argentina lililopangwa kufanyika keshokutwa kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Kenyatta, imefahamika.

Mwakinyo kwa sasa ananoa makali yake chini ya kocha, Tony Bellew, kutoka Liverpool, England ambako alikuwa kambini chini ya ufadhili wa Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya SportPesa.

Mbali ya Mwakinyo, pia Bellew anamfundisha bondia mwanamke, Fatuma Zarika ambaye atapambana na Catherine Phiri wa Zambia katika pambano la ubingwa wa dunia wa uzito wa Super Bantamweight ambao unatambuliwa na Baraza la Ngumi za Kulipwa Duniani (WBC).

Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema jana kuwa Mwakinyo anafanya mazoezi chini ya uwezeshaji wa kampuni yao.

Tarimba alisema kuwa mbali ya kampuni yao kuwezesha kambi ya Mwakinyo na Zarika, pia Bellew amevutiwa sana na viwango vya mabondia hao na wanaamini kuwa watafanya vizuri katika mapambano yao.

Alisema kuwa mabondia hao wamepata mafunzo bora na ya kisasa kutokana na umuhimu wa pambano hilo.

"Wakiwa mjini Liverpool, Mwakinyo na Zarika walijiandaa vyema kwa kuwa wanajua ugumu wa mapambano yao. Kampuni ya SportPesa imeona umuhimu huo na lengo letu kubwa ni kuona mabondia hao wanapata matokeo mazuri na kuwafurahisha wadau wa ngumi za kulipwa katika nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki," alisema Tarimba.

Alisema kuwa Gonzalez alitarajiwa kuwasili Kenya leo na kesho Ijumaa mabondia wote hao watapima uzito kwenye Hoteli ya The Stanley.

Pia mabondia hao watatembelea ofisi za SportPesa na kufanya mahojiano kwenye vituo mbalimbali vya televisheni na redio mbali ya kula chakula cha jioni na wafanyakazi wa kampuni hiyo.



Bondia Mtanzania, Hassan Mwakinyo, akiwasili jijini Nairobi Kenya, akitokea kambini England, alipokuwa akijiandaa kwa ajili ya pambano lake dhidi ya Eduardo Gonzalez kutoka Argentina litakalofanyika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Kenyatta keshokutwa. **PICHA: SPORTPESA**

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.AZAM | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.SIMBA | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4.LIPULI | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.KINONDONI MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.MTIBWA SUGAR | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ PRISONS | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.COASTAL UNION | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.MBEYA CITY | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.ALLIANCE | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.MWADUI | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.KAGERA SUGAR | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT TANZANIA | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.MBAO | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.STAND UTD | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.RUVU SHOOTING | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.SINGIDA UTD | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.NDANDA | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.BIASHARA UTD | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.AFRICAN LYON | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# SOS sasa kujenga viwanja Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIJIJI cha kulelea watoto yatima cha SOS visiwani hapo kinatarajia kuanza kujenga viwanja viwili vya michezo ili kuzipa fursa timu zao kuweza kujiandaa vema katika michezo ambayo imekuwa ikishirikisha shule mbalimbali.

Ujenzi wa viwanja hivyo umefadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia taasisi yake ya GIZ ambayo inajishughulisha na utoaji wa misaada katika sekta ya michezo kwenye nchi za Afrika.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini na makabidhiano juu ya ujenzi wa viwanja hivyo, Ofisa Utawala na Rasilimali Watu wa SOS, Salum Abdurahman, alisema watajenga viwanja vya kisasa ambavyo vitaweza kutumiwa na timu mbalimbali za ndani na nje ya kituo hicho ambazo zitahitaji kuvitumia.

Abdulrahman alisema katika ujenzi huo utazingatia zaidi vipimo vinavyohitajika katika sheria za soka, lakini hakutakuwa na majukwaa mengi kama ilivyo viwanja vingine vya kisasa ambavyo vinatumika kucheza mechi za ligi na mashindano mengine ya kimataifa.

"Viwanja hivi vitatusaidia sana hususan kwa timu zetu za hapa hapa shuleni, wanafunzi watapata fursa ya kujiandaa katika michezo hasa mpira wa miguu, ambapo muda mwingine tunakuwa na mechi za kirafiki kutoka shule mbalimbali," alisema kiongozi huyo.

Naye Mshauri Mkuu wa taasisi hiyo ya Ujerumani, Ali Salum, ambaye anashughulikia miundombinu, alisema madhumuni ya ujenzi huo ni kusaidia maendeleo ya michezo Afrika na tayari wameshajenga viwanja katika nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania Bara.

Kiongozi huyo alisema ujenzi wa uwanja huo unatarajiwa kuwa wa miezi miwili na kuongeza kuwa msaada huo umekuja muda mwafaka, ambapo serikali kupitia Wizara ya Elimu na ile inayoshughulikia michezo iko katika mpango wa kuvifufua viwanja vya michezo vilivyopo katika shule mbalimbali ili kuanza kutengeneza wanamichezo bora kuanzia ngazi za chini.

# Twiga Stars yaanza kuiwinda DR Congo

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha wachezaji 27 wa Timu ya Taifa ya Wanawake "Twiga Stars", kinatarajia kuanza mazoezi rasmi kesho kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Michezo ya Olimpiki dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) utakaochezwa Aprili 5, mwaka huu, hapa jijini Dar es Salaam.

Timu hiyo inayofundishwa na Bakari Shime pamoja na Edna Lema itasafiri kwenda DRC kwa ajili ya mchezo wa marudiano utakaochezwa Aprili 9, mwaka huu.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Lema aliliambia gazeti hili jana kuwa katika kujiandaa na mechi hiyo, wanatarajia kucheza mechi mbili za kirafiki ili kujiimarisha zaidi.

"Kambi itaanza leo (jana), lakini mazoezi tutaanza Ijumaa kwa sababu kuna wachezaji ambao wanatoka mikoani, ila muda tulionao utatosha kujipanga kuwakabili DRC," alisema kocha huyo.

Wachezaji walioitwa kujiandaa na mchezo huo ni pamoja na Fatuma Omar, Najiath Abbas (JKT Queens), Gelwa Migomba (Kigoma Sisters), Wema Richard (Mlandizi Queens), Maimuna Hamis (JKT Queens), Enekia Yona (Alliance Queens), Fatuma Issa (Evergreen), Fatuma Khatibu, Happyness Hezron, Stumai Abdallah, Anastazia Antony, Fatuma Bushir, Zena Khamis wote kutoka JKT Queens.

Wengine ni Grace Tony wa Yanga Princess, Mwanahamis Omari (Simba Queens), Donisia Daniel (JKT Queens), Asha Shaban (Kigoma Sisters), Asha Rashid (JKT Queens), Amina Ally (Simba Queens), Irene Elias ( Kigoma Sisters), Fatuma Mustapha (JKT Queens), Dotto Tossy (Simba Queens), Aisha Khamis, Esther Mabanza (Alliance Queens), Tausi Abdallah (Mlandizi Queens), Niwael Khalfan (Marsh Academy na Amina Abdallah kutoka Simba Queens.